# Nipashe

Ijumaa Agosti 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581028

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**CALVERT-LEWIN KUIKOSA CHELSEA**

UKURASA 22


BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,019,301,493/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mbaroni** tuhuma za mauaji ya mwanafunzi wa Chuo Kikuu DSM

UKURASA 3

# Bei za mafuta zaacha maumivu bidhaa sokoni

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### ORYX KUWEKEZA ZAIDI KWENYE GESI YA KUPIKIA

KAMPUNI ya ORYX Energies Tanzania imesema itaendelea kuwekeza zaidi kwenye mitambo ya kuhifadhi na kusambaza gesi ya kupikia (LPG), ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati ya kupikia ambayo ni rafiki kwa mazingira...

UKURASA WA 4

### MCT: POLISI, TCRA WAONGOZA MIGOGORO KWA WAANDISHI

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limefanya tathmini ya hali ya uhuru wa vyombo vya habari nchini, kuanzia Julai hadi Julai, mwaka huu na kubaini kuwa Jeshi la Polisi linaongoza kwa migogoro na waandishi wa...





Mfanyabiashara wa nafaka mbalimbali katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, Amani Ramadhan, akiweka vizuri bidhaa yake ya ufuta jana, ambapo bei yake imepanda kutoka 5,500/- hadi 6,000/- kwa kilo moja. Picha ndogo; Mchele mzuri umepanda bei kutoka 2,500/- hadi 2,800/- kwa kilo moja. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wagombea Kenya wabuni mbinu mpya kusaka kura

UKURASA 19

## Serikali yafufua mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo

UK. 2

**MICHEZO** **NABI AWATULIZA YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali yafufua mchakato ujenzi Bandari ya Bagamoyo

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imeanza mchakato wa kutafuta mwekezaji mpya kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo baada ya mazungumzo na mwekezaji wa awali kutokufikiwa mwafaka na hatimaye kujitoa.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema hayo jana alipoulizwa swali na waandishi wa habari kuhusiana na hatua ambayo serikali imefikia katika mpango wake wa kuanza ujenzi wa bandari hiyo.

"Bandari ya Bangamoyo ni kweli muda mrefu tumeizungumza na tulikuwa tunaenda vizuri na baadhi ya watu lakini sasa hivi inaonekana yale mazungumzo hayakwenda vizuri. Mwenyewe ameamua hatoendelea kuwekeza huko," alisema Prof. Mbarawa.

Pia alisema hata baada ya mazungumzo na mwekezaji wa awali kuvunjika, nia ya serikali ya kujenga bandari hiyo iko pale pale.

"Nia ya serikali iko pale pale kwa sababu tunajua bandari hii ya Dar es Salaam inaanza kufika mahali inashindwa uwezo wake na bandari itakayotuokoa ni hii ya Bagamoyo. Kwa hiyo hilo la serikali tunalijua na tutahakikisha tunalisimamia ili tuijenge haraka iwezekanavyo.

"Katika mpango huu, naamini tutapata wawekezaji wengine wazuri na wenye uwezo wa kujenga bandari hii ya Bagamoyo," alisema Mbarawa.

Wakati wa Bunge la Bajeti lililomalizika Juni 30, mwaka huu, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2022/23, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema katika kipindi cha mwaka 2021/22, serikali ilifufua majadiliano ya mradi wa Bandari na Kanda Maalum ya Bagamoyo (BSEZ) uliosimama tangu mwaka 2018.

Alisem wizara yake ndiyo ilikuwa inaratibu uendelezaji wa BSEZ unaolenga kuendana na ushindani wa biashara za usafiri wa majini pamoja na kuunganisha shughuli zingine za kiuchumi ikiwamo viwanda na utalii.

Dk. Kijaji alisema wizara hiyo ilifufua majadiliano na wawekezaji ambao ni Merchants Holdings (International) Co. Ltd (CMHI) ya China na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman (OIA) ambayo awali ilikuwa inaitwa Mfuko wa Uwekezaji wa Serikali ya Oman (SGRF).

Kwa mujibu wa Kijaji, majadiliano hayo yalihusu eneo dogo la mradi wa BSEZ kwa kuendeleza eneo la hekta 3,087 kati ya hekta 9,887 ambapo unahusisha ujenzi wa bandari.

Pia alisema mpango huo ulihusisha ujenzi wa kituo cha usafirishaji kwenye eneo la hekta 887 na uendelezaji wa eneo maalum la viwanda kwenye eneo la hekta 2,200.

# Bei mafuta yaacha maumivu sokoni

**Na Halfani Chusi**

NI maumivu. Hiyo ndiyo hali halisi ambayo iko katika masoko mbalimbali ya Dar es Salaam kutokana na kupanda kwa bidhaa kunakotoka na ongezeko la bei za mafuta ya petroli na dizeli zilizotangazwa juzi.

Nipashe ilitembelea masoko ya Buguruni, Kisutu na Mabibo na kubaini kupanda kwa bidhaa mbalimbali hususan vyakula kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kutokana na ongezeko la gharama za kusafirisha mazao na bidhaa za vyakula kutoka shambani hadi sokoni.

Kwa mujibu wa baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa hizo, kupanda huko kwa gharama za usafirishaji kumewalazimu kuongeza bei.

Mfanyabiashara katika soko la Kisutu anayeuza pilipili hoho, Mbidu Mbidu, alisema kwa bei jumla, kilo moja ya zao hilo imepanda kutoka Sh. 4,000 hadi Sh. 7,000.

"Sasa hivi hizi pilipili hoho za rangi mwanzoni kilo moja ilikuwa Sh. 4,000 lakini kwa sasa zimepanda mpaka kufikia Sh. 7,000. Kwa hizi za kijani mwanzoni kilo moja ilikuwa Sh. 1,000 lakini sasa hivi zinauzwa kwa Sh. 2,000 na bado bei inaendelea kuongezeka," alisema.

Masudi Shabani anayeuza dagaa, alisema bei ya bidhaa hiyo imeongezeka kwa sababu ya kupanda mafuta na kuongeza kuwa kwa sasa si msimu wake, hivyo wanapatikana kwa bahati nasibu.

"Dagaa kabla hata ya ongezeko la mafuta zilikuwa juu kutokana na dagaa kuwa na msimu wake na huu si msimu wake. Yalipoongezeka mafuta bei na dagaa pia wameongezeka bei. Kwa mfano mwanzoni dagaa wa Bukoba waliuzwa Sh. 5,000 kwa kilo.

"Lakini baada ya ongezeko la mafuta, kilo moja imefika Sh. 10,000 lakini pia dagaa wa nyama wa Zanzibar walikuwa wanauzwa Sh. 7,000 kwa kilo na hivi sasa bei imeongezeka hadi kufikia Sh. 10,000. Kuna mabadiliko makubwa ya bei kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta," alisema.

Naye Hassan Zungu anayeuza ndizi katika soko la Mabibo, alisema kabla ya ongezeko la mafuta, alikuwa anauza mkungu kwa Sh. 15,000 lakini sasa anauza Sh. 30,000.

"Bei bado inaendelea kupanda, hatujui kesho kutakucha vipi. Ndizi moja tulikuwa tunauza Sh. 250 lakini sasa tunauza Sh. 500, hivyo mfanyabiashara wa chipsi atauza bei ya juu zaidi ili apate faida. Ukiangalia hapo maisha yanazidi kuwa magumu bidhaa zinazidi kupanda bei kila siku," alisema.

Danieli Kugute, anayeuza mchele katika soko la Buguruni, alisema amelazimika kupandisha bei ili apate faida kidogo kutokana na kupanda kwa gharama za usafirishaji. "Mwanzoni mchele daraja la kwanza nilikuwa ninauza Sh. 1,900 kwa kilo lakini sasa nauza Sh. 2,700. Hii ni bei kubwa lakini hakuna namna. Ukiangalia gharama za usafiri hapo ukiuza chini ya bei hiyo, huwezi kupata faida kwa hiyo lazima uuze kwa bei ya juu zaidi," alitanabaisha.

Baadhi ya wanunuzi wa nyanya, vitunguu, karoti, nyanya chungu na bamia walisema wamelazimika kupandisha bei kutokana na kuongezeka kwa bei kutoka kwa wauzaji wa jumla.

Neema Mrisho alisema awali walinunua tenga la nyanya kwa Sh. 25,000 hadi 35,000 na wakati wa msimu halisi walinunua kwa Sh. 18,000 huku rejareja ikiuzwa kilo Sh. 1,500 hadi 2,500, lakini kwa sasa wananunua Sh. 45,000 na kwamba wanaenda kuuza rejareja kati ya Sh. 5,000 na 6,000 kwa kindoo cha lita tano, maarufu kama sado.

Mununuzi wa bidhaa hizo, Mwajuma Shabani, aliiambia Nipashe kuwa bei zimepanda kuliko matarajio huku akiomba serikali kuangalia uwezekano wa kudhibiti bei za mafuta.

Naye muuza chipsi aliyejitambulisha kwa jina la Babu Ally alisema ameshindwa kununua ndizi kwa sababu hajajua kama wateja wangu wataridhika na bei ya Sh. 1,000 mtaani kwake.

"Mwanzoni tulikuwa tunanunua ndizi moja Sh. 250 sokoni lakini sasa ndizi Sh. 500 ili na mimi nikapate faida lazima niuze zaidi ya Sh. 500. Sasa je, wateja wataelewa kweli?" Alihoji.

Dereva wa gari la mizigo linalofanya safari kati ya Mbeya na Dar es Salaam, Watabili Kigula, alisema kutokana na kupanda kwa mafuta, wamelazimika kuongeza gharama kutoka Sh. milioni 1.9 hadi Sh. milioni 2.2.

Rems Chonzi, dereva anayesafirisha bidhaa kutoka Iringa hadi Dar es Salaam, alisema amepandisha bei ya kusafirisha mizigo kutoka Sh. 900,000 hadi Sh. milioni 1.1 au milioni 1.2.

**TABOA YAFUNGUKA**

Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kimesema kinaangalia uwezekano wa kuishawishi serikali kuhusu upandaji wa mafuta mfululizo kwa sababu kinaona huduma itakuwa ngumu.

Akizungumza na Nipashe jana Mkurugenzi wa Habari wa TABOA, Mustapher Mwalongo, alisema kiuhalisia hali ni mbaya baada ya mafuta kupanda mfululizo.

"Tunaona huduma yetu itakuwa ngumu kuitoa lakini tunaangalia namna ya kuishawishi serikali ili iliangalie suala hili la upandaji wa mafuta mfululizo kwa mapana yake," alisema.

Mwalongo alisema jana walitarajia kufanya kikao lakini kutokana na akidi kutotimia kitafanyika baada ya wajumbe wote kutoka mikoa mbalimbali kufika mkoani Dar es Salaam.



Mkuu mpya wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kushoto), akikabidhiwa nyaraka na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, ambaye amehamishiwa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ikiwa ni ishara ya kukabidhiana ofisi, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Mitaala vyuo polisi ipitiwe'

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, ameviagiza vyuo vya polisi nchini kupitia upya mtaala wa mafunzo, kubaini kwa kiasi gani unajibu changamoto za utendaji kazi kwa maofisa na askari kwenye jamii.

Aidha, alisema baadhi ya askari wanaliaibisha jeshi hilo kutokana na tabia zisizofaa, hali inayoifanya jamii kujiuliza kama walipita kwenye mafunzo.

Akizungumza jana baada ya kukagua miradi ya Jeshi la Polisi katika Chuo cha Taaluma ya Polisi na Kikosi cha Mbwa na Farasi, Kurasini jijini Dar es Salaam, alisema kutokana na hali hiyo ni lazima kuangalia kama mitaala inakidhi matakwa.

"Nimewapa changamoto, wao ndiyo Chuo cha Maofisa na viongozi wa jeshi letu, nimewataka waangalie mtaala wao kwa kiwango gani unajaribu kugusa changamoto tunazoziona katika utekelezaji kazi wa maofisa na vijana wetu askari polisi, kwasababu hawa ndiyo viongozi, watuongezee mambo ya weledi itakayoweza kutusaidia vijana wanaohitimu," alisema na kuongeza:

"Ili wawasaidie wale askari wanaotoka kwenye kozi zile za msingi watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa PGO (Kanuni za Jeshi la Polisi) na maadili mema."

Kwa mujibu wa Waziri Sagini, wamekubaliana na viongozi wa chuo hicho kuwa na mkakati wa kuimarisha mafunzo pamoja na ufuatiliaji kwa wanaofunzwa kama wanatekeleza wajibu wao.

Aidha, Sagini aliridhishwa na kazi ya ujenzi wa mabweni manne katika chuo hicho ambayo yapo hatua ya mwisho kukamilika japo kuna ucheleweshaji wa miezi mitatu hadi mitano.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo hicho, SACP Lazaro Mambosasa, alisema licha ya chuo hicho kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma na ujenzi wa miundombinu, bado kinakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa miundombinu katika eneo jipya la mafunzo la mbinu za kivita lililoko wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani.

# Mbaroni tuhuma mauaji mwanafunzi UDSM

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia mkazi wa Ubungo Riverside, Gadi Daudi (28), maarufu Tito Jeshi la Mtu Mmoja, kwa tuhuma za mauaji ya mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Julius Fredrick (22).

Mtuhumiwa huyo anadaiwa amewahi kufungwa miaka 30 jela kwa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kuachiwa huru Aprili, mwaka huu, kwa sababu za kisheria baada ya kukata rufani.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema jana kuwa tukio hilo la mauaji ya wanafunzi lilitokea Julai 16, mwaka huu, saa 10:00 usiku karibu na hosteli za Magufuli Wilaya ya Ubungo.

Alisema mtuhumiwa huyo alimvamia Fredrick na kumshambulia na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili na baada ya tukio hilo, alimpora vitu vyote alivyokuwa navyo, ikiwamo simu.

"Baada ya ufuatiliaji, Julai 27, mwaka huu, Jeshi la Polisi lilifanikiwa kumkamata mtuhumiwa eneo la Sinza na alipohojiwa alikiri kumuua mwanafunzi huyo na kumpora vitu alivyokuwa navyo.

"Mtuhumiwa huyu amekiri kufanya matukio kama hayo ya unyang'anyi kwenye maeneo tofauti jijini Dar es Salaam. Tumebaini amekuwa akifanya matukio ya kihalifu maeneo ya Mlimani City, Mwenge na Kawe.

"Amewahi kushtakiwa kwa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha kesi namba 256/2020 na kufungwa miaka 30 kuanzia Julai 6, 2020 na aliachiwa huru Aprili, 2022 baada ya kukata rufani," alisema Muliro.

Kamanda Muliro alisema Agosti Mosi, mwaka huu, saa 10:00 jioni mtuhumiwa alikubali kuwapeleka polisi kuonyesha alipoficha silaha anazotumia katika uhalifu na simu ya marehemu aliyoipora.

Alisema vitu hivyo alikuwa amevificha kichakani eneo la katikati ya Mlimani City na hosteli za Magufuli.

"Baada ya kufika eneo la tukio, mtuhumiwa huyu alikurupuka na kuanza kukimbia kwenda kwenye vichaka vya ndani zaidi. Askari walifyatua risasi tatu hewani kumtahadharisha kusimama, lakini alikaidi na kulazimika kumzuia kwa risasi iliyomjeruhi kwenye paja la mguu wa kushoto," alisema.

Kamanda Muliro alisema mtuhumiwa huyo alianguka na kukamatwa na kupelekwa hospitalini na katika eneo la tukio polisi wamepata panga moja, sime, bisibisi na simu mbili za mkononi.

"Jeshi la Polisi linaendelea na msako kuwakamata wahalifu wote wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu. Lengo ni kuhakikisha watu wanafanya shughuli zao katika mazingira salama bila hofu kwa kuzingatia sheria," alisema.




Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Anne Makinda (katikati), akibonyeza kompyuta mpakato, kuzindua kampeni ya kuhamasisha Sensa ya Watu na Makazi Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, iliyoandaliwa na viongozi wa dini na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo, juzi. Kutoka (kushoto) ni Father Benno Kukudo wa Kanisa Katoliki, Mkuu wa Mkoa huo, Abubakar Kunenge, Mkuu wa Wilaya hiyo, Sara Msafiri na Shekh wa Mkoa huo, Hamis Mtupa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ORYX kuwekeza zaidi kwenye gesi ya kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ORYX Energies Tanzania imesema itaendelea kuwekeza zaidi kwenye mitambo ya kuhifadhi na kusambaza gesi ya kupikia (LPG), ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati ya kupikia ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Kalpesh Mehta, alisema hayo jana katika Kongamano la Kimataifa la Nishati 2022 lililoanza juzi jijini Dar es Salaam.

"Tunaendelea kukuza utangazaji wa mtandao wetu ili kufanya kila nyumba ya Mtanzania kuwa na nishati safi ya kupikia. Tutaendelea kuwekeza kwenye mitungi, usambazaji na uhifadhi wa gesi ya kupikia," alisema.

Mehta alisema kampuni hiyo imewekeza jumla ya dola milioni 20 nchini kuhakikisha upatikanaji wa gesi ya LPG unaongezeka ili kuwasaidia Watanzania waachane na matumizi ya kuni na mkaa ambayo ni tishio kwa mazingira.

Alibainisha kuwa kampuni hiyo ambayo ina asilimia 60 ya soko la gesi ya kupikia nchini, inashirikiana na Wizara ya Nishati kuhakikisha mabadiliko hayo yanafanyika, pia kutengeneza fursa za kibiashara miongoni mwa Watanzania kuhusu usambazaji wa LPG na biashara za rejareja.

Mehta alisema kampuni hiyo pia imeanzisha ruzuku ya mitungi ya LPG yenye uzito wa kilo 6 ili kuwezesha kaya kubadilika kutoka kwenye matumizi ya kuni na mkaa kwenda katika matumizi ya gesi katika upishi kwa kuwa gharama za awali ndizo zinazowakwamisha Watanzania wengi kutumia LPG.

"Tunashirikiana na washirika ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanatumia nishati hii safi kwa kupunguza gharama za awali kwa punguzo la hadi asilimia 70 ya bei ya jiko na mtungi uliojazwa," alisema.

Alisema kwa sasa mtungi wa kilo sita ambao unatumiwa zaidi na Watanzania walio wengi, unagharimu Sh. 85,000 lakini kampuni hiyo imetoa punguzo la bei ili kuwawezesha Watanzania wengi kumudu gharama.

Alisema kampuni hiyo pia inatoa ruzuku ya hadi asilimia 50 ya gharama za awali za LPG ili kuwawezesha wananchi wengi kufurahia nishati ya kupikia ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Mkurugenzi huyo alibainisha kua kila mwaka kampuni hiyo inatumia dola milioni 10 kwa biashara ya LPG ambapo nusu ya gharama hizo hutumika kama ruzuku. Alisema kuwa kwa sasa wana jumla ya mitungi ya milioni 2.5 sokoni.

Matumizi ya kuni na mkaa yanatajwa kuchangia miti mingi kukatwa na kusababisha uharibifu wa mazingira nchini.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Upatikanaji wa Nishati iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2016, asilimia 88.2 ya kaya za Mkoa wa Dar es Salaam zinatumia mkaa kama nishati huku asilimia 94.3 ya kaya za Mkoa wa Simiyu zikitumia kuni, jambo linaloashiria kuchangia uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa hewa ukaa.

# Bwege aenda Kenya kumpigia kampeni Odinga

**Na Romana Mallya**

MBUNGE mstaafu wa Kilwa Kusini, Selemani Bungara, maarufu Bwege, yupo nchini Kenya kumpigia kampeni mgombea wa urais wa Chama cha Ushirikiano wa Azimio la Umoja, Raila Odinga.

Bungara ambaye katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 aligombea jimbo hilo kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, amejipatia umaarufu kutokana na vibwagizo vyake alivyokuwa akivitoa wakati akichangia mijadala bungeni.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya kuwasili nchini Kenya, Bungara alisema atakuwapo huko mpaka Agosti 9, mwaka huu.

Alisema kilichowashawishi hadi kuitwa kwenda kumfanyia kampeni Odinga ni namna alivyoweza kusimamia uhuru, haki na demokrasia na vibwagizo vyake alivyokuwa akivitoa bungeni wakati wa uwasilishaji taarifa mbalimbali.

Alipoulizwa kwa nini mgombea huyo na sio mwingine, alisema Odinga ni baba wa mageuzi, mpigania haki za Wakenya asiyekata tamaa na mwenye lengo la kuwaunganisha wananchi kuwa wamoja.

Kuhusu tofauti ya uchaguzi wa Kenya na Tanzania, alisema, "utofauti ni mkubwa, Katiba ya Kenya inaendana na demokrasia ya mfumo wa vyama vingi vya siasa, wakati wa kampeni vyama vipo huru, sheria zinasimamiwa kwa usawa na haki tofauti na Tanzania usawa hakuna.

"Wakati wa kampeni Tanzania, chama tawala wanafanya watakavyo vyama vya upinzani wagombea wanaenguliwa bila kufuata sheria kanuni na taratibu vinakandamizwa kwa kuingiliwa kwa kuzuiliwa mikutano ya kampeni," alidai. Bungara alisema wanachoweza kujifunza na kukifanya Tanzania kwanza ni uwapo wa Katiba mpya ya wananchi itakayoendana na demokrasi ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Pia, alisema uwapo wa Bunge la Wananchi lenye kuisimamia, kuishauri na panapohitajika kuiwajibisha serikali na kuwa na mahakama huru na tume huru na huru kweli.

"Watawala wakubali kwa dhati ya moyo kwamba Tanzania ni nchi huru na ya kidemokrasia hivyo isimamiwe na itekelezwe," alisema.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa ACT-Wazalendo, Janeth Rithe, ilisema Bungara aliondoka jana kuelekea nchini Kenya kwa ajili ya kazi hiyo.

"Bwege ndiyo mwanasiasa wa kwanza kutoka Tanzania kupewa heshima hiyo na timu ya kampeni ya Azimio la Umoja. Kumbukumbu za mtandaoni zinaonyesha kuwa hotuba za Bwege ndani na nje ya Bunge zinafuatiliwa na kupendwa sana Kenya," alibainisha.




Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Nasri Ali (wa pili kushoto) na Meneja wa NMB Tawi la Mkuranga, Peter Masaki, wakifungua pazia kuzindua kongamano la 'Mwalimu Spesho' wilayani humo jana. Kutoka (kulia) ni Meneja Mwandamizi Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Ally Ngingite, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mwantum Mgonja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakuu wa mikoa, wilaya wapigwa marufuku kuondoka vituo vya kazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, ameagiza wakuu wa mikoa, wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya pamoja na wakurugenzi wa halmashauri wasitoke kwenye maeneo yao ya kazi hadi sensa ya watu na makazi itakapokamilika.

Bashungwa alitoa agizo hilo jana jijini hapo alipokuwa akielezea umuhimu wa sensa na uhusika wa sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ili kufanikisha itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

"Sensa ni muhimu kwa kuwa takwimu na sensa ndilo chimbuko la kuandaa mipango ya maendeleo ya nchi. Kutokana na umuhimu huu, viongozi hawa hawapaswi kutoka kwenye maeneo yao hadi wafanikishe hili. Iwapo kuna dharura lazima nipate taarifa ya dharura hiyo," alisema.

Viongozi hao, alisema watapaswa kuondoka kwenye maeneo yao kwa kibali maalum cha waziri kwa kuwa sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zina jukumu la kuhakikisha zinashirikiana na Kamati ya Uratibu wa Sensa Kitaifa ili ifanikiwe kwa asilimia 100.

Aliwataka wakuu hao kuhakikisha wanasimamia sensa kwenye mikoa yao na kutatua kero zitakazojitokeza badala ya kuweka malimbikizo ya kero.

"Naagiza makatibu tarafa, watendaji wa kata na vijiji, waheshimiwa madiwani, wenyeviti wa vijiji na vitongoji kuendelea kutoa ushirikiano kikamilifu kwa viongozi ambao wanasimamia sensa katika maeneo yao ili kuhakikisha inafanikiwa kwa asilimia 100," alisema.

# MCT: Polisi, TCRA waongoza migogoro kwa waandishi

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limefanya tathmini ya hali ya uhuru wa vyombo vya habari nchini, kuanzia Julai hadi Julai, mwaka huu na kubaini kuwa Jeshi la Polisi linaongoza kwa migogoro na waandishi wa habari ikifuatiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Pia, limebaini matukio ya ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari yamepungua kwa kiwango kikubwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Kajubi Mukajanga, kanzidata ya MCT ilirekodi matukio 10 ya madhila ambayo waandishi wa habari walikutana nayo 14 ya ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari.

Kati ya matukio hayo, matatu ni ya vyombo vya habari kufungiwa, tukio moja ni la kunyanyaswa, matatu ni kukamatwa, kunyimwa taarifa na mawili ni ya waandishi wa habari kutishiwa na mengine ni ya vitisho vilivyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na moja la watu wasiojulikana.

"Madhila hayo kwa mwaka jana kufungiwa lilikuwa moja, udhibiti hasi binafsi moja, kukamatwa manne, kunyimwa taarifa mawili, mauaji moja, vifaa kuharibiwa moja na vitisho matukio manne," alisema Mukajanga.

Kwa mujibu wa kanzidata ya MCT, kipindi cha mwaka 2020, ilirekodi matukio ya ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari 43 wakati mwaka 2021, ilirekodi matukio 25.

"Kwa jinsi hali ilivyo hivi sasa, matukio hayo yamepungua kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na miaka iliyopita. Tumekuwa tukishuhudia mabadiliko kutoka kwa utawala wa sasa ambao umeanzisha mchakato wa kupitia sheria za vyombo vya habari ili kurekebisha sheria kandamizi kwa uhuru wa vyombo vya habari," alisema Mukajanga.

"Kuthibitisha hilo, Februari 10, mwaka huu, wakati akitoa leseni kwa magazeti manne yaliyokuwa yamefungiwa, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliweka wazi kuwa kufunguliwa kwa vyombo vya Mawio, Tanzania Daima, Mseto na MwanaHALISI yalikuwa ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan."

Alisema mabadiliko hayo ni ishara kwamba ilikuwa ni kutokana na utayari wa serikali kwa mawaziri kufanya mazungumzo na wadau katika sekta hiyo.

"Hapo awali tulishuhudia msururu wa sheria mpya zilizotungwa, wakati mwingine kwa hati ya dharura, na ambazo zilikandamiza uhuru wa vyombo vya habari, ambazo ni pamoja na Sheria ya Uhalifu wa Mtandaoni, 2015 na Kanuni zake za 2016, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016.

Nyingine ni Kanuni za EPOCA (Maudhui ya Mtandaoni) 2018. Kitu ambacho kwa sasa hakionekani kujitokeza na sheria hizi hizi ziko katika mchakato wa kubadilishwa," alisema Mukajanga.

"Kubadilika kwa hali hiyo kunasababishwa na utayari wa kiongozi mkuu wa nchi ambaye ameonyesha kuithamini tasnia ya habari na kuwa tayari kufanya nayo kazi. Matamshi ambayo yanatolewa na viongozi hasa wanaosimamia tasnia ya habari ni dalili tosha kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wa tasnia ya habari tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo waandishi wa habari walionekana kama maadui wa serikali."

Alisema watahakikisha sekta hiyo inaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha sheria zote kandamizi zinafanyiwa marekebisho.

"Kitu kikubwa cha kuzingatia ni kuhakikisha tunaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha sheria zote kandamizi zinafanyiwa marekebisho. Tasnia ya habari inapaswa kukumbuka kuwa sheria kandamizi bado zimo vitabuni. Haki ya raia kujieleza na kupashana habari ni haki ya msingi na haipaswi kutegemea tu nia njema ya kiongozi aliyeko madarakani."

"Wakati tukimpongeza Rais kwa kuonyesha nia ya kuleta mabadiliko, hatupaswi kubweteka, tuendelee kusukuma mbele mchakato wa kubadilisha hizi sheria. Bila sheria kubadilika kicheko tulichonacho hivi sasa kunaweza kuwa cha muda mfupi."

# Chongolo aagiza ujenzi stendi ya Moshi ukamilike

**Na Mary Geofrey,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amemtaka Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, kupanga namna ya kumaliza ujenzi wa stendi ya mabasi wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Chongolo alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza kwenye mkutano wa ndani wa viongozi na wanachama wa CCM Wilaya ya Moshi, katika mwendelezo wa ziara yake ya siku tano mkoani Kilimanjaro ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/25 na kuhimiza ushiriki wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Alisema wizara zote mbili zikae na kupanga namna ya kupata fedha za kumalizia mradi huo uliokaa muda mrefu bila kukamilika.

"Wananchi hawataki maneno, hawataki hadithi, wananchi wanachotaka huduma inayokusudiwa itolewe kwa wakati. Tuliahidi kuwajengea stendi, ujenzi umeanza fedha zimebakia kiasi fulani," alisema Chongolo.

Aliipongeza serikali ambayo imeshatoa Shilingi bilioni saba kwa ajili ya kazi hiyo kati ya Sh. bilioni 17 zinazohitajika na kwamba kiwango hicho kimepungua kutoka Sh. bilioni 27 zilizokuwa zinahitajika awali kabla ya kupunguza majengo ya hoteli yaliyotakiwa kujengwa.

"Hii stendi lazima ikamilike, iondoke kuwa hadithi iwe stendi ambayo itaanza kutumiwa na wananchi wa mkoa huu hususani wananchi wa halmashauri ya Moshi wanufaike na stendi hii ya kisasa mapema iwezekanavyo," aliagiza Chongolo.

Aliahidi kulifuatilia kwa karibu suala hilo na kwamba alishaongea na Bashungwa ambaye alimuahidi kuwa wanalifanyia kazi kufuatilia Hazina ili watoe fedha utekelezaji uendeee.

"Niwahakikishie naenda na agizo langu litawafikia kabla sijafika, sisi ndiyo wenye ilani hatupo tayari kusubiri tena mpaka 2025 kuja tena kuulizwa kuhusu stendi ya mabasi.

"Tunataka stendi ya Moshi ikamilike, watu waanze kuitumia, tuanze mipango mingine na tuachane na hadithi ya muda mrefu. Nimepewa dhamana ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan na yeye hawezi kukubali kukutana na maswali ambayo majibu yake ni rahisi na utekelezaji tu," alisema.

Alifafanua zaidi kuwa, hawawezi kuendelea kuvumilia kukaa na miradi ya kwenye makaratasi na badala yake ni utekelezaji.

# Ashtakiwa kujiwasilisha kama Rais Samia

**Na Grace Gurisha**

MJASIRIAMALI Nickson Mfoi (20), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akituhumiwa kwa mashtaka mawili likiwamo la kujiwasilisha kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Ashura Mnzava, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate wa mahakama hiyo kuwa mshtakiwa huyo ambaye ni mkazi wa Mkoa wa Mwanza katika shtaka la kwanza, alitenda Septemba 22, 2021 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nia ya kulaghai umma akijiwasilisha kama Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika shtaka la pili inadaiwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Oktoba 2, 2021 kwa kukutwa akitumia laini ya simu iliyokuwa ikimilikiwa na Getness Jackson bila kutoa taarifa kwa mtoa huduma.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo alikana kuhusika na tuhuma hizo na upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

Wakili Mnzava aliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali (PH).

Hakimu Kabate alisema ili mshtakiwa awe nje kwa dhamana anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwaminifu na mwenye kazi ambayo inaaminika akiwa na kitambulisho cha taifa.

Hata hivyo, mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti ya dhamana na kurudishwa rumande hadi Septemba 18, mwaka 2022.



Mkulima wa matunda ya Strawberry, Lina Humphrey, akivuna zao hilo shambani kwake, Kata ya Nsalaga, jijini Mbeya jana. Tunda hilo huliwa lakini hutumika kutia ladha katika aina mbalimbali za vyakula na kuweka rangi, harufu na nakshi katika vipodozi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# ACT-Wazalendo yatoa neno gharama kuunganisha umeme

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimetoa mapendekezo kwa serikali ikiwamo kufutwa kwa gharama za kuunganisha umeme kutoka kwa wananchi na badala yake ibebe kupitia kodi zinazolipwa na wananchi.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Sekta ya Nishati wa ACT-Wazalendo, Isihaka Mchinjita, ilisema chama hicho kinaiomba serikali kuboresha utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo.

Alisema chama kimekuwa kikifuatilia kwa karibu utekelezaji wa uamuzi wa serikali kurudisha gharama za awali za kuunganisha umeme na kwamba wananchi kubebeshwa gharama hizo ni kikwazo kupata nishati hiyo hasa kwa wale wa kipato cha chini wakiwamo wa vijijini.

"Gharama ya kuunganisha umeme katika umbali wa mita 30 kwa njia moja ilikuwa Sh. 27,000 kwa vijijini na kwa sasa ni 320,960 mijini. Gharama ya Sh 27,000 ilionekana kuwa nafuu na kuwavutia wengi kutamani kuunganishiwa umeme majumbani kwao," alisema na kuongeza;

"Utekelezaji una sura tofauti ambapo mwananchi hulazimika kulipia gharama zingine zaidi pale umbali unapozidi mita 30 kwa wastani wa Sh. 300,000 kwa kila nguzo moja inayozidi."

Aliongeza kuwa sababu za kushushwa kwa gharama za uunganishaji wa umeme ni kutokana na wananchi wengi kushindwa kumudu gharama za kuunganisha, akieleza kuwa hoja hiyo haiwezi kufa kwa sababu ya mwananchi kuwa mbali ya mita 30.

Pia alisema takwimu zinaonyesha usambazaji wa umeme vijijini hadi kufikia Aprili, 2021 vijiji 10,312 viliunganishiwa ikilinganishwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa mwaka 2015 ikiwa ni ongezeko la vijiji 8,294 sawa na asilimia 86 ya vijiji vya Tanzania Bara.

Alibainisha kuwa hali ya usambazaji kwa sasa ni tofauti na matumizi ya umeme kwenye kaya, kwa mujibu wa utafiti wa Tanzania invest 2021 unaoonyesha kuwa asilimia 24 ya watanzania wanatumia huduma ya umeme.

"Hii ni kusema kwamba, umeme umefika vijijini kwa asilimia 86 kama inavyosemwa na serikali, lakini watanzania wanaomudu au walioweza kuvuta umeme kwa ajili ya matumizi ya majumbani ni asilimia 24 pekee," alisema.

Pia alisema ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/21 inakazia hoja ya kuchelewesha kwa kuonyesha kuwa wateja hucheleweshwa kuanzia siku saba hadi 481.

Alisema chama hicho kimepokea malalamiko kutoka mkoani Lindi na Tanga juu ya mwenendo usioridhisha wa utekelezaji wa Mradi wa REA kwenye kijiji cha kwashemshi Korogwe mkoani Tanga na Mahiwa mkoani Lindi.

# Chanzo migogoro ardhi Dar chatajwa

**Na Waandishi Wetu**

KAMISHNA Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam, Idrisa Kayera, amesema sababu kubwa ya kukithiri kwa migogoro ya ardhi mkoani humo ni uvamizi.

Kayera alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe katika ofisi ndogo za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambako wanaendesha kampeni maalumu ya kusikiliza malalamiko ya migogoro ya ardhi ngazi ya mkoa.

Alisema kampeni hiyo ni ya siku tano ambayo ilianza juzi na kwamba katika siku hizo ambazo wamesikiliza, malalamiko mengi ya migogoro yanahusu migogoro ya ardhi iliyovamiwa.

Pia alisema wamebaini baadhi ya migogoro hiyo inasababishwa na viongozi wa serikali za mitaa na kwamba tayari baadhi yao wamewachukulia hatua, ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

"Tumeanza kampeni hii inafanyika kwa siku tano kusikiliza malalamiko kuhusiana na migogoro ya ardhi. Tulianza na Temeke, Kinondoni, Kigamboni, Ubungo na tutamalizia na Ilala kesho (leo). Baada ya kusikilizwa, wananchi watajibiwa kwa barua," alisema.

"Migogoro ya ardhi katika mkoa wa Dar es Salaam kwa kiwango kikubwa imepungua, miongoni mwa kazi kubwa zilizofanyika kupunguza migogoro hiyo ni kuboresha kumbukumbu za umiliki wa ardhi.

"Kwamba hati na ramani zote zimeingizwa kwenye mfumo wa kielektroniki, na mji wote umepigwa picha ili kurahisisha kuona kila ardhi au kiwanja chochote kilichopo kwenye mkoa huu, kama kimejengwa, kimepimwa, kimemilikishwa au la," aliongeza.

Alisema jambo jingine ambalo limechangia kupunguza migogoro ni kwenda kwenye maeneo ya wananchi kuwasikiliza na kuwapatia hati miliki pamoja na kurasimisha maeneo yao. Kayera alisema kwa sasa zaidi ya asilimia 70 ya mkoa wa Dar es Salaam umepimwa.

Pia alisema pamoja na kupungua kwa migogoro ya ardhi katika mkoa huo, bado kuna maeneo ambayo yamevamiwa na kwamba tayari wameanzisha kampeni maalumu ya kuwaondoa wavamizi katika yote yaliyovamiwa katika mkoa huo.

"Uvamizi ni kosa la jinai na watu wasivamie maeneo. Watu kama hawa hakuna cha kuwasaidia isipokuwa ni kuwachukulia hatua na kuwaondoa katika maeneo waliyovamia.

"Yako makundi makubwa ya watu ya kuanzia hata 300 na kuendelea ambayo yamekuwa yakienda kwenye maeneo ya ardhi na kuvamia na haya ndio yanasababisha kuendelea kuwapo na migogoro ya ardhi kwenye mkoa huu," alisema.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo yamevamiwa na makundi hayo makubwa ya watu kuwa ni Mabwepande, Pugu, Mbondole, Tuangoma, Kibada na Nyakasangwe.

"Hapo nyuma tulifanya utaratibu wa kuwakutanisha wavamizi na wavamiwa, ili waone kama wanaweza kuwalipa, lakini tumeona suala hili litakuwa donda sugu na litatuletea shida baadae, kwa hiyo tumeachana nalo, tunawaondoa kwa sababu wengi wameendelea kuvamia wakiamini kwamba wakishafanya hivyo watarasimishwa."

Alitaja maeneo mengine makubwa yaliyovamiwa kuwa ni la Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) lililoko Mabwepande, la Wizara ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mwasiliano, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Kibada Block II,

Alisema oparesheni hiyo ya kuondoa wavamizi ina miezi miwili tangu imeanzishwa na tayari kwa wilaya ya Kinondoni pekee wameondoa zaidi ya wavamizi 150.

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR) na Loyce Cyriacus (SJMC).**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada za haraka zinahitajika kunusuru kupanda kwa bidhaa

**BEI** ya mafuta kwa sasa iko juu, imesababisha kuongezeka gharama kwa wananchi na kasi ya ugumu wa maisha kwa kiwango kikubwa kutokana na bei za bidhaa kuwa juu au kwa lugha rahisi mfumuko wa bei.

Juzi, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ilitangaza bei mpya ambazo zimepanda kwa kiasi kikubwa katika historia ya Tanzania, maana yake inakwenda kuathiri moja kwa moja maisha ya Mtanzania wa kipato cha chini.

Kwa mujibu wa EWURA bei ya rejareja mkoani kwa mafuta ya petroli kwa sasa inauzwa Sh. 3,410 kutoka Sh. 3,220, dizeli Sh. 3,322 kutoka Sh.3,143 na mafuta ya taa Sh. 3,765 kutoka Sh. 3,442 kwa lita.

Kupanda kwa bei ya mafuta moja kwa moja kumeathiri Watanzania wengi wanaoishi katika maisha duni ambao wengi wao wanategemea kula mlo mmoja au miwili kwa siku.

Kwa siku ya jana katika masoko makubwa kwenye Jiji la Dar es Salaam kama Soko la Kisutu bei ya bidhaa zilikuwa juu.

Hata katika vyombo vya usafiri nauli zimeongezeka tangu bei ya mafuta ilipoongezeka miezi miwili iliyopita, bodaboda, bajaji, daladala zote zimepandisha nauli.

Suala la kupanda bei za nauli kwa vyombo vya usafiri kupitia ongezeko la bei ya mafuta limeongeza kwa kasi na kusababisha ugumu wa maisha mitaani.

Maumivu ni makubwa kwa watu wenye vipato vidogo na waswahili wanasema, kipato kwa sasa hakikidhi mahitaji, kwa maana ya kuwa kinachopatikana hakimudu gharama za matumizi.

Tunaamini serikali yetu ni sikivu na kilio hiki cha wananchi cha kupunguza makali ya maisha kitasikika.

Kadhalika, tunaamini kwamba ni jambo la heri na muhimu kwa maofisa wa serikali wenye dhamana na suala hili wakaingilia kati, kwani litawasaidia Watanzania wote na hasa wenye vipato vidogo katika jitihada za kumudu mahitaji na kurejesha tumaini jipya la mtaani ambako kuna kundi kubwa la umma.

Imani yetu kwa serikali ni kuharakisha kushuka kwa bei ya mafuta, kwa kuwa hali ni mbaya mtaani kwa kufanya hivyo kutapunguza gharama za maisha na kuongeza mzunguko wa pesa mtaani.

Tunatambua wizarani kuna kitengo cha biashara, ambacho hufuatilia bei za bidhaa kila siku kwenye mikoa mbalimbali na kutoa taarifa, lakini bado haijasaidia kupunguza bei.

Tanzania kuna wasomi wengi wa uchumi wanaoweza kushauri nini kifanyike kuwapunguzia wananchi makali ya maisha, bila kulazimisha wafanyabiashara ambao wanawajibu wa kulipa kodi kupunguza makali.

Kwa nchi zilizoendelea serikali huweka ruzuku kwenye bidhaa ili kuwasaidia wananchi wasiumie na wauzaji wasipate hasara, lakini kwa nchi zetu ni ngumu zaidi ya kufuatilia kwa karibu hali ya soko ili kuona kama bei sio ya maumivu.

Ni wajibu wa serikali kufuatilia kwa karibu hali kwenye masoko na maduka ili kuona bei zinaendana na uhalisia, kwa kuwa wakiachwa kuna uwezekano wa wafanyabiashara kujipanga kuwa na msimamo wa bei ambao unawatengenezea faida kubwa, huku ikiamsha umuhimu wa kuwa na umoja wa walaji na kutetea maslahi ya wengi.

Tunashauri hivyo kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa katika nchi zinazoendelea hakujawa na uelewa kuhusu mfumo wa soko huru, hivyo tusishangae hata muuza muhogo shambani kwake akipandisha bei kwa kisingizio cha mafuta.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mnangoja kutumbuliwa ndipo mkomeshe lumbesa?

Na Beatrice Moses

**NI** maadhimisho ya Siku ya Wakulima au Nanenane ambayo yanafikia kilele chake kila mwaka Agosti 8. Pamoja na maonyesho na mauzo ya bidhaa mbalimbali za wakulima, kujitangaza na kutandaa (networking) changamoto zao nazo huibuliwa.

Wakulima ni tegemeo kubwa kwa nchi mbalimbali kwa kuwa ndiyo wazalishaji wa mazao kuanzia ya chakula na biashara, wanyama na rasilimali za viwandani, hata hivyo kwa sababu mbalimbali hasa wakulima nchini wanajikuta kwenye nyakati ngumu kipindi cha kuvuna na kuuza mazao yao.

Ni tatizo linalowakumba kutokana na shinikizo ambalo wamekuwa wakilipata kutoka kwa wafanyabiashara wakiwamo madalali wa mazao wanaotajwa kuwa huwalazimisha kuwauzia bidhaa kweye ujazo zaidi au kwa uwingi zaidi na huo ndiyo mwanzo wa lumbesa.

Lumbesa ni kujaza mazao zaidi ya kipimo kilichowekwa kwenye gunia, kiroba na ndoo ni kujaza na kushindilia hadi kumwagika, jambo linalofanywa kwa makusudi ili mnunuzi apate zaidi tena kwa kulazimisha na kumuumiza mkulima, anayepata kiduchu tofauti na mavuno ya mazao wanayouza.

Serikali kwa muda mrefu imeliona hilo ambapo viongozi kadhaa wa ngazi tofauti wamejitokeza kulikemea na limeripotiwa kwenye vyombo vya habari mbalimbali na kupigwa marufuku lakini bado mkulima anaumizwa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Agosti mwaka jana akiwa katika kijiji cha Ilolo kilichoko kata ya Kiwira mkoani Mbeya alizungumza na wananchi katika eneo hilo ambao miongoni mwa mazao wanayolima ni viazi mviringo ambavyo pia vinafungashwa kwa utaratibu wa lumbesa.

Katika mazungumzo hayo Waziri Mkuu hakusita kuzungumzia lumbesa na kukemea kuwa ni wizi kwa wakulima, hivyo akatoa maagizo kwa Wizara ya Kilimo kusimamia matumizi ya mizani hasa kwenye masoko ya vijijini .

> **Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Agosti mwaka jana akiwa katika kijiji cha Ilolo kilichoko kata ya Kiwira mkoani Mbeya alizungumza na wananchi katika eneo hilo ambao miongoni mwa mazao wanayolima ni viazi mviringo ambavyo pia vinafungashwa kwa utaratibu wa lumbesa.**

Jambo hilo limezungumzwa na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akiwa kwenye maonyesho ya Nane Nane wiki hii mkoani Morogoro, akisema ununuzi wa mazao kwa lumbesa, uishe na mazao yote yanunuliwe kwa vipimo vya mizani na si vinginevyo.

Ni wazi kuwa serikali imesikia kilio cha wakulima kuhusu kipimo hicho, ambacho ni wazi ukitafakari kinawasababishia mateso na umasikini kwa kuwa hawanufaiki ipasavyo ikilinganishwa na nguvu walizotumia kuandaa, kupanda hadi kuvuna mazao hayo.

Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba licha ya viongozi kupiga marufuku bado magunia ya lumbesa ya aina mbalimbali yamejaa sokoni, hapo ndipo kuna zua maswali je viongozi wa masoko hawatambui hilo na kushiriki kudhibiti? Je Wizara ya Kilimo na Biashara zinafanya juhudi gani kukomesha jambo hilo ili kumkomboa mkulima dhidi ya wizi huu wa wazi?

Ifike wakati wahusika wawajibishwe ili mkulima apate haki yake kwa kuwa hadi lini viongozi wataendelea kupaza sauti jambo hili lidhibitiwe lakini kumekuwa na hali ya kusuasua katika kulikomesha, kilio cha wakulima siyo cha samaki kwamba machozi yanaondoka na maji, kwa kuwa wao ni miongoni mwa watu tegemeo kwa afya na uchumi wa taifa kwa ujumla.

Sasa isisubiriwe kusikia Rais Samia Suluhu Hassan, naye anapiga marufuku jambo hilo, hatua zinazostahili zichukuliwe, watendaji waone umuhimu, kulikomesha na kumaliza tatizo hilo sasa.

Sheria ya kupiga marufuku upakiaji wa mazao na bidhaa kupita ujazo au uzito katika magunia ipo tangu mwaka 2016, je haina 'meno'? Inahitajika kuona umuhimu wa uwepo wake katika nchi kwa kusaidia wakulima. Ni vyema sheria hiyo itumike ipasavyo kukomesha lumbesa.

# LATRA yaongeza muda wa tiketi za kielektroniki

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema imeongeza muda wa mwezi mmoja kuanzia Agosti mosi hadi 31, mwaka huu, kwa mabasi ambayo hayajajiunga na mfumo wa kukatisha tiketi kielektroniki, wajiunge.

Imesema mabasi ambayo hayatajiunga na mfumo huo ndani ya muda huo, adhabu yake itakuwa faini ya papo kwa hapo ya Sh. 250,000 kwa watakaokiri kosa, huku wasiokiri kosa watapelekwa mahakamani na faini ni kati ya Sh. 300,000 hadi 500,000.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, aliiambia Nipashe kuwa uamuzi huo umetokana na mwitikio mkubwa kwa mabasi hayo ndani ya siku sita tangu walipotangaza tarehe ya ukomo Julai 31.

"Wakati tunatoa taarifa ya ukomo Julai 26, ni mabasi 550 tu ndiyo yalikuwa yamejiunga na mfumo huo. Ndani ya siku tano mpaka Julai 31, yalifika mabasi 1,432, mwitikio ni mkubwa sana. Ndiyo maana tumeona tusifanye haraka kutoa adhabu, bali tuwape muda tena ili tukianza kutoa adhabu wajue kuwa wamezembea," alisema Suluo. Alisema muda wa nyongeza utakuwa ni kwa ajili ya kufanya tathmini kuangalia changamoto wanazokutana nazo watumiaji.

Mkurugenzi huyo alisema, wanategemea kufanya kikao na wadau wa usafiri huo ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kujadili namna bora ya kuyasaidia mabasi 2,482 ambayo hayajajiunga ili nayo yawe kwenye mfumo huo.

"Tunashukuru ile taarifa yako ulioitoa jana imetusaidia kutambua kuwa kumbe mawakala wengine mashine wameziweka mezani wanaendelea kutoa tiketi za zamani. Hii inaonyesha kuwa kuna baadhi ya mawakala bado huu mfumo hawajaukubali, wamezoea kushika fedha zao mkononi badala ya kupeleka benki, kwa hiyo tutaendelea kuelimisha," alisema.

Kwa mujibu wa Suluo, mabasi yaliyosajiliwa kusafirisha abiria mikoani ni 7,572 mabasi yanayotoa huduma ya usafiri ni 3,912, wakati 3,660 hayatoi huduma hiyo ingawa hayajatoa taarifa rasmi ya kusitisha shughuli hiyo.

Alisema lengo la kuleta mfumo huo ni kuwasaidia wafanyabiashara wapate faida sahihi na kuwapunguzia abiria mzigo wa kulipa fedha nyingi zaidi ya bei elekezi kutokana na uwapo wa mawakala wanaopandisha bei.

Mapema wiki hii, Nipashe ilitembelea baadhi ya ofisi za wakala wa mabasi yaendayo mkoani katika Kituo cha Magufuli, Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam na kubaini mashine hizo kutotumika huku utoaji tiketi ukiendelea wa utaratibu wa zamani.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akimsikiliza Meneja Masoko wa Benki ya Stanbic Tanzania, Joseph Mhaiki (kushoto), kuhusu huduma zinazotolewa na benki hiyo kwa wakulima kwenye banda la benki hiyo, viwanja vya John Mwakalange mjini Mbeya. Benki hiyo inaunga mkono jitihada za serikali katika kuleta mafanikio ya kilimo nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabwawa 10 kujengwa maeneo ya ukame

**Na Thobias Mwanakatwe,** CHEMBA

SERIKALI imeanza kutekeleza ujenzi wa mabwawa 10 kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua ambayo yatagharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.5 katika maeneo yenye ukame ili kukabiliana na ukosefu wa huduma hiyo.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alisema hayo baada ya kukagua ujenzi wa bwawa linalojengwa katika kijiji cha Kelema lililokamilika kujengwa kijiji cha Paranga wilayani Chemba huku akibainisha kwamba kati ya mabwawa hayo, sita yatajengwa katika mkoa wa Dodoma.

Aweso alisema mabwawa hayo yatajengwa katika vijiji vya Ombiri,Jambi ya Nyasa, Patanga na Kelema katika wilaya ya Chemba na katika wilaya ya Bahi yatajengwa katika vijiji vya Mpamantwa na Uhelela.

Serikali, alisema inajenga mabwawa katika maeneo ambayo ni makame ili kuwawezesha wananchi kupata huduma ya maji safi na salama ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kumtua ndoo mama.

"Mvua inayonyesha nchini kwetu iwe fursa na si maafa. Kwa hiyo maji yatakayokuwa yanavunwa kwenye mabwawa haya yatatumika katika kilimo na kunywa," alisema.

Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Dk. George Lugomela, alisema katika mwaka ujao wa fedha yatajengwa mabwawa mengine 11 baada ya kupata Sh. bilioni sita.

Dk. Lugomela alisema ujenzi wa mabwawa haya ni moja ya motisha ya kuboresha upatikanaji wa maji kwa wananchi waliopo katika maeneo ya vijijini hususani yaliyo na ukame wa kipindi kirefu.

"Lengo kubwa la ujenzi wa mabwawa haya ni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, umwagiliaji wa bustani,pamoja na mifugo," alisema.

Dk. Lugomela alisema mabwawa yatakapokamilika yatawanufaisha watu 14,908 na mifugo 67,084 katika wilaya ya Chemba na katika wilaya ya Bahi watanufaika watu 13,767 na wanyama 24,063.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa Mabwawa katika Wizara ya Maji, Domina Msonge, alisema mabwawa yanayojengwa Chemba na Bahi yatakamilika yote ndani ya mwaka huu na kwamba ujenzi wa bwawa moja unachukua wiki tatu hadi kukamilika.

# TBL yaanzisha kampeni unywaji salama

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) imezindua kampeni yake ya unywaji bia salama iliyoanza Agosti Mosi, mwaka huu, ikiwa na nia ya kuwaelimisha wanywaji na kuwakumbusha hatua za unywaji salama wa bia.

TBL pamoja na kampuni mama, AB InBev wamechukua jukumu la kusaidia kupunguza matumizi hatarishi ya pombe ulimwenguni. Mwaka 2015, AB InBev ilizindua malengo ya dunia ya unywaji salama ambayo yanatarajiwa kufikiwa mwishoni mwa mwaka 2025.

Uadhimishaji wa Wiki ya Unywaji Salama ya mwaka huu umelenga kubadilisha baadhi ya tabia hatarishi za unywaji zilizozoeleka na kuhamasisha unywaji salama kwa lengo la kuhakikisha wanywaji wanafurahia bia kila mara bila kupata athari.

Kupitia kampeni hiyo, uongozi wa TBL umesema unahamasisha unywaji salama kwa kuhimiza wanywaji kuzingatia kunywa maji katikati ya kunywa bia, kula chakula wakati wa kunywa na kuita usafiri wa kurudi nyumbani mapema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran, alisema jana kuwa: "TBL inataka kuwapa wateja wake wote dondoo za unywaji salama kwa kuwa tabia ya unywaji salama imekuwa sehemu ya utamaduni wa TBL na AB InBev na tungependa kuiendeleza na kuileta kwenye jamii.

"Unywaji salama ndiyo unatufanya tufurahie bidhaa zetu kila mara. Unywaji salama ni zaidi ya kunywa kistaarabu, kwani unaruhusu wanywaji kufurahia bia zao kwa kiwango cha juu zaidi."

Alisema ili kufikia malengo ya kampeni hiyo na kuhamasisha unywaji salama, TBL imeshirikiana na chapa mbalimbali za bia zake ili kuwafikishia wateja ujumbe na kuwaelimisha.

Mkurugenzi huyo alisema kwa Tanzania, TBL imelenga kuwashirikisha vijana wanaoruhusiwa kunywa kisheria, kuhamasisha tabia ya unywaji salama kupitia bia zake zinazopendwa na wengi.

"Kupitia chapa mbalimbali za bia za TBL, ujumbe wa unywaji salama utaweza kuwafikia wengi zaidi na kupunguza matumizi hatarishi ya pombe na vilevi," alisema.

# SHIVYATIATA yalaani wanafunzi kuogeshwa dawa mvuto mapenzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Tiba asili Tanzania (SHIVYATIATA) limelaani tabia ya baadhi ya waganga wa jadi kuwaogesha wanafunzi wa kike dawa za mvuto wa mapenzi ili waolewe wakiwa na umri mdogo.

Mratibu wa Shirikisho hilo Kanda ya Magharibi, Athumani Waziri, alisema jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu waganga wa jadi wanavyokamatwa na nyara mbalimbali za serikali zikiwamo ngozi za chui na mikia ya wanyama, zinazotumika katika kazi zao.

Alisema kitendo cha mganga wa tiba asili kuwarubuni wazazi na kuwaogesha dawa za mvuto wa mapenzi wanafunzi wa kike (samba) ni kinyume cha taratibu za kazi zao na katika eneo lake, atayebainika awatajibika kisheria.

"Tunaungana na serikali kupinga vikali tabia ya namna hii ndani ya jamii zetu kwa sababu hazikubaliki, zinadhalilisha na zinaharibu ndoto za wanafunzi, hivyo tuungane kuwaibua waganga wa jadi wenye tabia kama hizo na kuwaripoti katika mamlaka husika," alisema waziri.

Pia alisema awali wakunga wa jadi walituhumiwa kuwapatia dawa za kuongeza uchungu wajawazito hali ambayo ilifanya kuwa na vifo vya wajawazito na watoto wachanga na walilikemea hadi likaisha na hilo litakwisha kwa kufanya mikutano mbalimbali na kukumbusha wajibu wao.

Waziri aliwasihi waganga wa tiba asili kusajili shughuli zao na kupata vibali vya kufanya kazi katika hali ya usalama na kuondokana na kukamatwa mara kwa mara na Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na kuzilipia nyara za serikali wanazozitumia katika kazi zao.

Mratibu wa Tiba Asili katika Halmashauri ya Ushetu, Allex Silayo, aliwatahadhirisha waganga hao kupokea vyeti vya kughushi kwa kuwa ni kosa kisheria na badala yake wafike katika ofisi husika zinazojihusisha na usajili wa tiba asili na kujisajili.

Alisema mganga atakayebainika kuwa na cheti chenye usajili wa kugushi atawajibika kisheria ili iwe ufundisho kwa wengine na kuwataka kuwa na tabia ya kuhudhuria vikao pale wanapowahitaji kwa sababu wanakuwa na ujumbe muhimu kutoka serikalini na kukumbushana wajibu wa kufanya kazi vyema.

Mmoja wa waganga wa jadi, Mabula Masanja, alisema baadhi yao wamesajili kazi zao na kupata vibali vya uendeshaji wa shughuli lakini bado wanakamatwa na vitendo hivyo vimekuwa vikifanyika nyakati za usiku na kuiomba serikali kuingilia kati na kutatua tatizo hilo.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2022/23. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TEA kutumia bil. 8.9/- kuboresha elimu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), katika mwaka wa fedha wa 2022/23 inatarajia kutumia Sh. bilioni 8.9 kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu nchini. Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Bahati Geuzye, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu majukumu ya taasisi hiyo na utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Alisema kiasi hicho cha fedha kitatumika kufadhili miradi 96 katika shule 96 za msingi na sekondari katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara pamoja na taasisi mbili za elimu ya juu Zanzibar.

Geuzye alisema miradi itakayofadhiliwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa 99, matundu ya vyoo 792, maabara kumi za masomo ya sayansi kwa ajili ya shule tano za sekondari, nyumba za walimu 52 na mabweni 10.

Mkurugenzi huyo alitaja miradi mingine itakayotekelezwa kuwa ni ujenzi wa miundombinu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum inayojumuisha madarasa 10, matundu ya vyoo 40 pamoja na mabweni mawili katika shule 6 za msingi na moja ya sekondari

Alisema pia katika mwaka huu wa fedha 2022/23 Mfuko wa Elimu wa Taifa utaboresha miundombinu na kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa taasisi mbili za elimu ya juu zilizoko Tanzania - Zanzibar na kwamba miradi hiyo imepangwa kutumia shilingi milioni 500 katika utekelezaji wake.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 ,TEA iliboresha na kukarabati baadhi ya shule za msingi ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi katika mji wa Dodoma ikiwa sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali za kuhamishia makao makuu kwenye mji huo.

Alisema mradi huo ulilenga kukarabati na kupanua miundombinu ya shule nne za msingi za Kizota, Medeli, Kisasa na Mlimwa C na shilingi bilioni 1.9 zilitumika.

Aidha, alisema TEA inafadhili ujenzi wa shule ya msingi ya Mchepuo wa lugha ya Kiingereza katika Jiji la Dodoma wenye thamani ya shilingi milioni 750, mradi ambao unasimamiwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Mkurugenzi hiyo alisema mfuko wa elimu pia umefadhili ujenzi wa jengo la Hanga kwa ajili ya mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege katika Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia, Zanzibar.

Alisema pia wametekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu na kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Utawala wa Umma Zanzibar.

# Kituo taarifa utalii chapata majisafi

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE kituo cha taarifa za utalii kinachosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani kimepata majisafi.

Huduma hiyo ya maji imesogezwa kwenye kituo hicho na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo jana, Meneja wa Mkoa wa Kihuduma DAWASA Kisarawe, Alexander Ng'wandu, alisema mradi huo umetekelezwa kwa lengo la kupeleka huduma ya maji safi kwenye eneo hilo ili kuondoa adha ya upatikanaji wa maji wakati huu wa ujenzi na wakati patakapokamilika na kuanza kutumika.

"Mahali hapa hapakuwa na huduma ya maji hivyo kuleta usumbufu kwa TFS kuendesha shughuli zao," alisema.

Ng'wandu alieleza kuwa kazi imehusisha ulazaji wa bomba la inchi 1.5 kwa umbali wa mita 300 na bomba la inchi 1 kwa umbali wa mita 150 kwenye eneo la msitu wa Kazimzumbwi.

Aliongeza kuwa mradi umetekelezwa kutoka kwenye bomba kuu la inchi 2.5 kwenda kwenye eneo hilo la TFS kwa umbali wa mita 450.

"TFS ni wadau wetu wanaochangia katika kuboresha mazingira na kuchochea utunzaji mzuri wa miundombinu ya maji, hivyo utekelezaji wa mradi huu ni sehemu mojawapo ya kuimarisha uhusiano baina ya taasisi hizi," alisema Ng'wandu.

Alisema kazi inaendelea na inatarajiwa kukamilika ndani ya siku tatu.

Mkandarasi wa ujenzi wa kituo hicho, Mhandisi Deogratius Mushi, alisema ujio wa maji kwenye eneo hilo ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwa kuwa itarahisisha utendaji wa kazi ya ujenzi unaoendelea.

Mushi alisema kazi ya ujenzi wa kituo hicho inahitaji maji mengi yanayopatikana kwa urahisi, maji ya kununua yanagharama sana tofauti na maji ya bomba kutoka DAWASA.

"Kwa kiasi kikubwa itapunguza gharama za kununua maji, maana kwa siku natumia lita 2,000 hadi 4,000 kwenye ujenzi, hivyo maji kutoka DAWASA yatasaidia kupunguza gharama," alisema.

Aliiomba DAWASA kutekeleza mradi huu kwa muda ili waanze kupata maji mapema na kuondokana na gharama kubwa za kununua maji.

# Watu 200,000 wachanja UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WANANCHI 238,000 kati ya 605,000 sawa na asilimia 38 mkoani Lindi, wamepata chanjo ya UVIKO-19 ya lengo lililowekwa.

Haya yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa kampeni ya kuhamasisha wananchi kuchanja katika viwanja vya Ilulu mjini hapo.

Kampeni ambayo iliandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na FHI 360 kupitia mradi wa Epic kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID).

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Dk. Kheri Kyage, alisema jitihada zinafanyika kuhakikisha wananchi wanajitokeza kwa wingi kuchanja na kwamba wanatarajia kufikia lengo.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi ambaye ndiye Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema kampeni hiyo inafanyika kwenye halmashauri zote za mkoa huo, na kwamba lengo ni kuhakikisha wanakuwa salama.

"Kama mnavyojua kuna habari ambazo si sahihi zimekuwa zikitolewa na baadhi ya watu ambao hawana nia njema kuhusu chanjo ya UVIKO-19. Hii ni moja ya sababu za Wizara ya Afya kuja na hii kampeni kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu chanjo hii. Natoa rai kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi kujitokeza kuchanja chanjo hii ni salama na haina madhara yoyote," alisema Ndemanga.

Pia alipongeza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, kuboresha afya za wananchi wake, ikiwamo kuongoza kampeni ya kuchanja na kuhakikisha inapatikana hadi maeneo ya vijijini.

Epic ni mradi wa kimataifa wa miaka mitano unaotekelezwa na Shirika la FHI360 kwa ufadhili wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) na USAID, uliojikita katika kufikia na kuendeleza udhibiti wa janga la VVU/UKIMWI.

Mradi huo una lenga kutoa msaada wa kitaalamu na huduma za moja kwa moja katika kuondoa vikwazo na kuhamasisha usimamizi wa kujitegemea wa miradi ya VVU/UKIMWI kitaifa kwa kuboresha programu za utambuzi wa hali ya maambukizi ya VVU, kinga, matunzo na tiba.

# Pikipiki zitumiazo nishati jadidifu kudhibiti ujangili

**Na Ashton Balaigwa, aliyekuwa BABATI**

TAASISI ya Uhifadhi ya Chemchem, inayofanyakazi katika Hifadhi ya Jumuiya ya Wanyamapori (WMA) ya Burunge, wilayani Babati mkoani Manyara, inakusudia kutumia pikipiki zisizo na mlio za nishati ya jua kudhibiti ujangili hifadhini.

Meneja Programu wa Chemchem, Hamisi Gyori, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kujifunza juu ya uwekezaji katika Hifadhi ya WMA ya Burunge na mkakati wa kudhibiti ujangili.

Waandishi waliotoka Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), kinachotekeleza mradi wa USAID wa Tuhifadhi Maliasili.

Alisema wameamua kusaidia mapambano ya ujangili kupitia vyombo vya usafiri wa pikipiki zitakazotumiwa na askari wanyamapori na kwamba zilitoka nchini Ujerumani na kugharimu Dola za Marekani 72,000.

Akielezea mfumo wa pikipiki hizo, alisema zinatumia betri za nishati ya jua.

"Sisi tumewekeza kwenye utalii wa picha na hoteli ndani ya Hifadhi ya Burunge, tumekuwa tukisaidia mambo mbalimbali ya kijamii ndani na nje hifadhi sasa katika mapambano ya ujangili tumeamua kutoa hizo pikipiki za kisasa kwa askari wa kikosi cha kudhibiti ujangili," alisema.

Gyori alisema awali walishatoa pikipiki za kawaida mbili na kwamba wanatarajia kufunga mitambo maalumu ya kisasa inayotumia satelaiti itakayokuwa na uwezo wa kubaini mienendo ya vyombo vya moto na watu wanaoingia hifadhini.

Katibu wa Jumuiya hiyo, Benson Mwaise, alisema vitendo vya ujangili vimekuwa vikifanyika zaidi nje ya hifadhi kutokana na wanyama kuvamia mashamba ya wananchi hasa kipindi cha ukame, lakini baadhi yao wamekuwa wakitoa taarifa na kudhibiti kwa haraka.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili umelenga kuboresha taarifa kuhusu utunzaji wa mapito ya wanyamapori maarufu kama shoroba.




Mtaalamu Mdhibiti Ubora wa Mradi wa kudhibiti sumukuvu Tanzania (TANIPAC), Mercy Butta (wa pili kushoto), akitoa maelezo ya namna kiuatilifu cha kibaiolojia kinachodhibiti ukuaji wa kuvu wanaozalisha sumukuvu shambani kwa wananchi waliotembelea banda lao, katika maonyesho ya wakulima Nanenane, yanayofanyika kitaifa viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TEMESA yadai bil. 9/- taasisi za umma

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Temeke imesema Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), unazidai taasisi za serikali Sh. bilioni tisa kutokana na kupatiwa huduma za matengenezo ya magari na ufundi umeme katika majengo yao.

Hayo yalibainishwa jijini Dar es Salaam jana na Mkuu wa TAKUKURU Temeke, Holle Makungu, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kwa kuanzia Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Alisema deni hilo ni la miezi mitatu na kipindi cha nyuma, huku akizitaka taasisi za serikali zinazodaiwa kulipa ili kuwezesha wakala kutekeleza majukumu yake na kabla hazijachukuliwa hatua.

"Tayari tumeshaanza kuyachunguza madeni haya ambayo yameisababishia TEMESA kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi. TAKUKURU Mkoa wa Temeke tumeshafanya kikao cha pamoja na wadaiwa hao na wametoa mapendekezo yatakayowezesha madeni hayo kulipwa. Tunashukuru baadhi ya taasisi zimeshaanza kulipa," alifafanua Makungu.

Pia alisema kwa kipindi hicho wamepokea malalamiko 29 ya rushwa na kwamba idara zinazolalamikiwa ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ardhi, Mahakama, Afya, Elimu, Polisi, Benki na sekta binafsi.

Alisema TAKUKURU Temeke ilifuatilia utekelezaji wa miradi 12 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.7 ya sekta ya ujenzi, elimu, afya na barabara, na kubaini kati yake 10 sawa na asilimia 83 ilicheleweshwa kukamilika kwa mujibu wa mkataba.

Kwa mujibu wa Makungu, kuchelewa huko kunasababisha ongezeko la gharama za ujenzi na pia walibaini kutumika vifaa visivyo na ubora pamoja na manunuzi zaidi ya bei halisi ya soko.

# NBC yawahakikishia wakulima bima kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeendelea kutoa huduma ya bima ya kilimo kwa wakulima kwa lengo la kuwapa uhakika wa kazi zao pamoja na uzalishaji.

Akizungumza kwenye maonyesho ya Nanenane jijini hapo, Mkuu wa Wateja Wadogo, Huduma ya Lariba na Wakulima wa NBC, Raymond Urassa, alisema ushiriki wa benki hiyo kwenye maonyesho hayo ni mwendelezo wa jitihada za kuwa karibu na wadau wa sekta muhimu.

"Kupitia maonyesho haya, tunapata fursa ya kutangaza huduma zetu zinazohusiana na sekta nzima ya kilimo pamoja na kupokea mrejesho wa huduma hizo kutoka kwa wakulima," alisema.

Urassa alisema ushiriki wa benki hiyo kwenye sekta ya kilimo unahusisha mkakati wa benki hiyo kuinua sekta ya kilimo nchini unaofahamika kama 'NBC Shambani' unaohusisha mnyororo wote wa sekta ya kilimo kuanzia kwa mkulima, mchakataji wa mazao ya kilimo hadi msambazaji.

"Zaidi pia tunalenga kuhakikisha tunashirikiana vema na serikali katika kutimiza adhma ya msingi kabisa ya kuhakikisha tunaongeza kwa kasi ukuaji wa sekta ya kilimo nchini ikiwa ni sambamba na kuboresha maisha ya wakulima wenyewe," alibainisha.

Akizungumzia baadhi ya huduma zinazotolewa na benki hiyo mahususi kwa wakulima,

Urassa aliitaja huduma ya bima inayotolewa kwa kushirikiana na kampuni ya bima ya Jubilee, inayolenga kuwalinda wakulima, wavuvi na wafugaji nchini dhidi ya hasara pindi wanapopata majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri uzalishaji wao.

"Benki ya NBC tuinatambua vema sekta ya kilimo na zaidi tunatambua mchango wa wakulima katika uchangiaji wa uchumi wa nchi na kwa msingi huu tumeona ni vema kuja na bima ya mazao kwa wakulima.

"Katika kuthibitisha ufanisi wa huduma hii, ni hivi karibuni tu kwa kushirikiana na wenzetu kampuni ya Bima ya Jubilee Insurance tuliwafidia wakulima wa tumbaku mkoani Tabora ambao mazao yao yaliathiriwa na hali ya hewa," alibainisha.

## Ukosefu elimu chanzo ukosefu wa tija zabibu

**Magdalena Jackson na Peter Mkwavila,** DODOMA

KUKOSEKANA kwa elimu kwa wakulima wa zabibu nchini kumetajwa kuwa sababu ya kukosa kwa tija ya zao hilo.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Armachius James, akizungumza jana na Nipashe kwenye maonyesho ya Nanenane jijini hapo, alisema asilimia kubwa ya wakulima hawana elimu juu ya aina gani ya zabibu wanatakiwa kulima kulingana na matumizi yake.

"Kuna aina tatu za zabibu, ambazo ni zabibu za mvinyo, matunda (zabibu za mezani) na zabibu za viungo. Wakulima wengi wanalima zabibu za mvinyo, hivyo kwa sababu ya kukosa elimu wanashindwa jinsi ya kuzihudumia," alisema.

Alisema kuwa zabibu ni zao linalohitaji sana jua ili kutengeneza sukari, hazihitaji mvua bali kwa maji ya kumwagiliwa ili zisisumbuliwe na fangasi. Alibainisha kuwa zabibu zinafaa kulimwa maeneo ya Dodoma, Singida, Tabora na Same.

Naye Ofisa Kilimo wa Taasisi hiyo, Sunday Mwinga, alisema kuna aina zaidi ya 60 za mbegu za zabibu zinazopatikana Makutupora.

Alitaja aina hizo ni Tintacao, Vranac, Palomino, Queen of vine yard , Rejina na Kismis craven ambazo baadhi yake ni za mbegu za mvinyo, matunda na viungo.

"Ili ufanikishe kilimo hicho unatakiwa usiache mmea wa zabibu usambae, hivyo wakulima wanapaswa kukatia mmea kila unapootea ili kuzaa. Zabibu inaweza kuvunwa kila baada ya miezi minne kama italimwa kwa kufuata utaratibu huo," alisema.

Pia alisema zabibu inajitengenezea amira yake yenyewe inayoonekana juu ya tunda hivyo katika utengenezaji wa mvinyo haitakiwi kuoshwa au kuongeza amira kwa sababu inajichachusha.

"TARI inaendelea kufanya utafiti wa mbegu mpya za zabibu kabla ya kuwasilisha kwa wakulima ili kujiridhisha juu ya ubora na viwango wa mbegu hizo," alisema na kuwashauri wakulima wa zabibu kuunda vikundi ili kuuza zabibu zao kwa ujumla katika viwanda vya mvinyo.




Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma PSSSF, James Mlowe (kushoto), akielezea ubora wa tangawizi iliyochakatwa (ginger powder) kwenye banda la PSSSF viwanja vya John Mwakangale. PSSSF imewekeza kwenye kiwanda cha kuchakata tangawizi cha Mamba Miamba Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro. **PICHA: KHALFAN SAID**

## PSSSF yaita wafugaji, wakulima kujifunza fursa

**Na Khalfan Said,** MBEYA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ambao unashiriki katika Maonesho ya Nanenane 2022 kwenye viwanja vya John Mwakangale, umewaalika wakulima, wafugaji na wavuvi, kutembelea banda lao ili kuona fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mfuko huo katika eneo la uwekezaji.

Pia kuona fursa za uwekezaji na kupeana mawazo mbalimbali ya maeneo ambayo PSSSF inaweza kuwekeza zaidi ili kuunga mkono nguvu za wakulima, wafugaji na wavuvi kuongeza thamani ya mazao yao na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma PSSSF, James Mlowe, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja hivyo, Agosti 4, 2022.


"Pamoja na majukumu mbalimbali tunayofanya ya kulipa mafao na kuandikisha wanachama, pia PSSSF tunafanya shughuli za uwekezaji ili kulinda michango ya wanachama na kuendelea kutimiza wajibu wetu wa kulipa mafao yatolewayo na mfuko," alisema.

Alisema katika kuunga mkono malengo ya serikali ya Agenda 10/30 ifikapo mwaka 2030 ukuaji wa sekta ya kilimo ufikie angalau asilimia 10, PSSSF tayari imeshaonyesha njia kwa kuanza kuwekeza katika viwanda mbalimbali vya bidhaa za kilimo na mifugo.

"Tumewekeza katika kiwanda cha kuchakata tangawizi kilichoko Mamba Miamba wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, machinjio ya kisasa Nguru Ranch Hills, yaliyoko wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro, lakini kiwanda kikubwa cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd (KLICL), kilichoko mkoani Kilimanjaro," alifafanua.

Alisema viwanda vyote hivyo vimeanza uzalishaji na matunda yameanza kuonekana kwa wakulima wa tangawizi hivi sasa kuwa na soko la uhakika la kuuza zao lao walilozalisha, pia wafugaji wa mkoani Morogoro na maeneo jirani nao wamepata sehemu ya kuuza mifugo yao ikiwamo ng'ombe, kondoo na mbuzi. Mlowe alisema, PSSSF kwa kushirikiana na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), wamewekeza kwa ubia katika kiwanda cha chai, Mponde Tea Plant kilichoko wilayani Lushoto mkoani Tanga.

"Kiwanda hiki tunatarajia kitaanza uzalishaji Novemba mwaka huu na hapa nataka niseme kiwanda hiki tayari kimeleta hamasa kubwa kwa wakulima kwani wataweza kuongeza thamani ya zao hilo kwa kuchakata chai tayari kwa kuuza kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema.




Ukurasa 13

LATRA mnaupiga wote, lakini pigeni na hapa

## Maonyesho ya ufugaji yalivyonoga na safari kuelekea zama za kufuga kisasa

Ukurasa 14




# BUFE

IJUMAA AGOSTI 5, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


BIASHARA

# Ni uwanja mpya wa batiki wazalishaji kuunganishwa

**Na Sabato Kasika**

- Kupimwa kama majora viwandani
- Siku ya kulienzi vazi hilo inakuja



Uzalishaji batiki unafanyika mahali popote. **PICHA: MAKTABA**

KUTENGENEZA na kuuza batiki ni moja ya ujasiriamali uliowatoa kiuchumi wanawake wa mikoa mbalimbali.Licha ya watu kuziona kama nguo duni zenye mabakabaka, zinabamba kwa watalii na wanaopenda masuala ya kitamaduni.

Ukifanywa na vikundi vidogo vya kinamama ni uwekezaji, unaofananishwa na usemi wa jembe halimtupi mkulima kwa jinsi ambavyo nguo hizo zilivyoboresha uchumi wa mwanamke.

Batiki si kama majora yanayozalishwa viwandani ambayo hutengenezwa kwa vipimo vinavyotambulika rasmi, nguo hizo huuzwa kwa vipande vyenye vipimo tofauti.

Lakini, Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na utaalamu wa kukuza na kuendeleza biashara za wajasiriamali wadogo ya Roijok Progress Centre, Rose Urio, anasema suala la kukosa vipimo liko mbioni kurekebishwa.

Anasema taasisi yake inataka kuunganisha wazalishaji wa batiki wa Tanzania na kuandaa vipimo vinavyofanana ili kuwa na masoko makubwa ya kuuza bidhaa hiyo nje na ndani ya nchi.

Anayasema hayo hivi karibuni katika hafla ya uzinduzi wa Siku ya Batiki Tanzania na kufafanua kuwa kumekuwapo na vipimo vya mita 2.5 hadi nne na sasa wanataka wakubaliane kuwa na vipimo vya aina moja.

"Tunakwenda kuboresha vipimo vya batiki.Hatuna vipimo vinavyolingana. Unaweza kukutana na mfanyabiashara ana mita mbili na nusu, mwingine tatu au nne, kwa hiyo tunahitaji kuwa na vipimo vya aina moja," anasema Rose.

Mkurugenzi huyo anaongeza kuwa ubora na viwango vya batiki hauna budi kwenda sambamba na vipimo vinavyolingana ili kufanikisha mfanyabishara kuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Kwa mujibu wa maelezo yake, hatua hiyo inakusudia kuwaunganisha wazalishaji wa batiki Tanzania kuwa na masoko makubwa ya kuuza bidhaa hiyo kwa wingi hasa ikiwa na vipimo na ubora unaolingana na kukubalika.

"Baada ya kupata vipimo na ubora vinavyohitajika, hatua hiyo itawezesha batiki kujiuza na kupata masoko mengi zaidi makubwa ndani ya nchi na nje na kumwinua mwanamke kiuchumi.

**VIPIMO KUTOFAUTIANA**

Mzalishaji na muuza batiki Nuru Diko, wa Manzese anatoa sababu za vipimo kutofautiana akisema ni kutokana na mahitaji ya wateja na kwamba wanaoshona mashati au blauzi, hununua vitambaa vya mita moja na nusu, lakini vya magauni vinaanzia mita mbili na nusu hadi tatu au nne kutegemeana na mwili wa mhusika.

"Hivyo, kwa hali hiyo, ni muhimu kuwapo kwa vipimo vya aina tofauti, lakini kwa kuwa tunataka kwenda mbele kupata soko la kimataifa, hatuna budi kwenda na wakati," anasema.

Kuhusu batiki kuyumbishwa na mitumba anasema siyo tishio kwa soko la batiki, kwa kuwa zina wateja maalum wakiwamo watalii na watu wanaofahamu umuhimu wa mavazi hayo.

"Kazi ya mikono kama hii ya kutengeneza batiki ina wateja maalum, hivyo ina soko lake na mitumba nayo ina soko lake, wala haiwezi kuwa tishio kwa batiki," anasema Nuru.

**SERIKALI KAZINI**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima ambaye anashuhudia uzinduzi huo, anasema serikali ipo kazini ili kuwakomboa wanawake katika shughuli zao mbalimbali za kiuchumi.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

# TARURA yasherehekea mafanikio miaka mitano kuanzishwa kwake

## • Yajayo mradi ujenzi bonde Jangwani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usimamizi wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) unaadhimisha miaka mitano tangu uanzishwe, ukiwa na mafanikio lukuki kiasi cha wengine kudhani umekuwepo nchini miaka mingi..

TARURA ilizinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Julai 2 ya mwaka 2017, baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali Mei mwaka huo.

Ni uzinduzi ambao Waziri Mkuu, alitamka katika lugha ya ahadi kwamba, itakabili changamoto ya usafiri nchini, hasa maeneo ya vijijini yaliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikielekea kumalizika.

"Wakala huu tunaouzindua leo, utakuwa na manufaa makubwa kwa ustawi wa nchi yetu kwa kuongeza chachu ya uzalishaji mali mashambani kutokana na urahisi wa mazao kufika sokoni. Utashusha bei ya vyakula mijini na bidhaa za viwandani vijijini, kutokana na gharama za usafirishaji mazao kutoka mashambani na bidhaa za viwandani kutoka mijini kupungua," anasema.



Daraja la chuma lililoko Kibiti mkoa wa Pwani

**MBUNGE AJIELEZA**

Je, kuna ishara gani ya kutumia aliyoyanena Waziri Mkuu Majaliwa, miaka mitano iliyopita? Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, anatoa maoni yake:

"Kabla ya TARURA kuifungua Halmashauri ya Ushetu kwa barabara zinazopitika kwa vipindi vyote vya mwaka hali ilikuwa ngumu sana.

"Tulikuwa tunalima, tunavuna sana lakini wakati mwingine unakuta tumbaku, mahindi pamoja na alizeti zetu zinakwama kutoka shambani, hivyo wakati mwingine wakulima huuza mazao yao kwa bei rahisi ili kukwepa adha ya usafiri," anasema

Anafafanua kwamba wakulima walikuwa wanatumia gharama kubwa ya kusafirisha mazao na hasa kipindi cha mvua, kwa sababu magari makubwa hayakuweza kuingia vijijini kuchukua mazao yao, kwa kuwa barabara zilikuwa za udongo, hata magari mengi hasa ya uzito mkubwa yanazama.

"Ilikuwa inatubidi tukodishe magari yenye uzito mdogo kwa ajili ya kusomba mazao kutoka shambani, kitu ambacho kilikuwa kikiongeza gharama za mazao huku, wakulima wengi wakishindwa kuzimudu," anasema.

> **"Kabla ya TARURA kuifungua Halmashauri ya Ushetu kwa barabara zinazopitika kwa vipindi vyote vya mwaka hali ilikuwa ngumu sana.**

BOSI MKUU

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Victor Seff, anasema lengo kuu la kuanzishwa Tarura ni kufanya matengenezo endelevu ya barabara na madaraja kwa gharama nafuu, ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya kijamii nchini.

"Wakala huu umeanzishwa ukiwa na dira ya kuwa taasisi inayoongoza katika menejimenti ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kupanga, kusanifu na kujenga kwa kuzingatia ufanisi wa gharama," anasema.

Seff anasema, TARURA ilipoanzishwa ilikuwa na mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 108,946.19, kati ya hizo, 56,624.59 zilitangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali.

Anasema walifanya utambuzi na uhakiki wa mtandao wa barabara za wilaya, ikiwa ni pamoja na kilomita 52,321.60 zilizokuwa hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na wakakamilisha.

Anasema, katika kipindi cha miaka mitano mtandao wa barabara wanazohudumia sasa una urefu wa km 144,429.77 na zote zimeshatangazwa kwenye gazeti hilo, toleo la Juni 25, 2021.

"Mtandao huo wa barabara ni ongezeko la kilomita 87,805.17 ambazo bado zilikuwa hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali," anasema.

Anaongeza kuwa kuna madaraja 3,191 na makalavati 69,317, barabara za lami kilometa 2,404.9, za changarawe kilomita 29,166.57 wakati za udongo ni kilometa 112,858.3.

Seff anasema, fedha kwa ajili ya uendeshaji na utekelezaji wa majukumu ya TARURA zitatokana na mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na wakala, serikali kuu, mfuko wa barabara na wadau wa maendeleo.

Anataja wadau hao ni Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID), Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na Umoja wa Ulaya (EU). Pia, anasema mamlaka za serikali za mitaa hutoa fedha za ujenzi na matengenezo kupitia mapato yao ya ndani.

Mhandisi Seff anasema, mpango mkakati wa kwanza wa Tarura ulianza kutekelezwa Julai Mosi, 2017 na kukamilika Juni 30, mwaka jana.

"Katika kipindi hicho, kuna barabara zenye urefu wa kilomita 24,979.24 zilifanyiwa matengenezo, kilomita 955.35 zilijengwa kwa kiwango cha lami na 16,857.82 ni za changarawe," anasema.

Pia, anayataja madaraja 231 yaliyojengwa kutoka madaraja 2,960, hadi 3,191 sambamba na makalavati 1,325 yamejengwa.

Katika kipindi hicho anasema ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo ya maegesho ya magari kwenye matumizi ya hifadhi ya barabara mapato yalifika Sh bilioni 50.41 toka Julai 2018 hadi Juni 2021.

Mtendaji huyo wa TARURA, anasema kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa ukusanyaji mapato ya maegesho, Tarura ilianzisha mfumo wa kielektroniki wa TARURA eRevenue Management Information System (TeRMIS).

Anasema, ni mfumo uliotengenezwa na wataalamu wa TARURA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, sasa unaonyesha mafanikio makubwa.

Seff akiorodhesha mafanikio zaidi katika miaka mitano anasema wameweza kuwa na jengo la makao makuu katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambalo tayari linatumika, akiutaja mwaka 2019 walisimika mfumo wa malipo serikalini (MUSE).

Anasema, umesaidia kuongeza udhibiti na usimamizi wa rasilimali fedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji na kudhibiti matumizi ambayo hayakuwapo kwenye mpango.

Aidha, kitengo cha usanifu na usimamizi wa utekelezaji wa kazi za barabara na madaraja kiitwacho TARURA Engineering and Environmental Consulting Unit, mpaka sasa kimefanya usanifu wa barabara zenye urefu wa kilometa 147.47 na madaraja 39.

Anasema, katika kuboresha makao makuu ya nchi, Tarura katika mji wa Magufuli, Mtumba wamejenga barabara za lami nzito zenye urefu wa km 51.2 kwa Sh 89,112,145,500.06

**MPANGO MKAKATI ll**

Baada ya kwisha mpango mkakati wa kwanza (2016/2017 - 2020/2021), TARURA imeandaa mpango wa pili wa miaka mitano kuboresha barabara za wilaya ukihusisha utunzaji barabara zilizo katika hali nzuri na za wastani kubaki katika hali hiyo.

Pia, anataja itahusisha kupunguza barabara zenye hali mbaya na kuziweka katika hali nzuri, ili zipitike mwaka mzima, kukiwa na matarajio mtandao wa barabara za lami miaka mitano ijayo utaongezeka.

Hapo kunatajwa kutoka kilomita 2,404.90 za sasa hadi kilomita 855.65, changarawe kutoka kilomita 29,116.57 hadi 102,358.14 na madaraja idadi yake 2,812, hadi 6,620 na fedha zitakazotumika kwenye mpango huo wa pili zinakadiriwa kuwa Sh trilioni 3.6.

Mratibu Humphrey Kanyenye, anayesimamia miradi hiyo chini ya TAMISEMI, kwa Fedha za Benki ya Dunia, akifafanua anasema wana mradi wa barabara kwa ajili ya kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii nchini baadhi zikitekelezwa na TARURA.

Mradi huo ulianza Julai Mosi mwaka jana na unatekelezwa kwa miaka sita kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 350, Dola milioni 300 zikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka benki ya Dunia na Dola milioni 50 ni mchango wa serikali.

Mradi huo anasema utahusisha ujenzi wa barabara za km 535 kwa lami huku barabara za km 400 zikiwa chini ya Tarura na kilomita 135 zitakuwa chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS).

Mradi huo pia unafanyia matengenezo sehemu korofi zenye urefu wa km 2,900 pamoja na matengenezo ya kawaida urefu wa km 23,000 katika barabara za Tarura.

Maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni barabara ya Wenda - Mgama kilomita 9 na Mtilili - Ifwagi kilomita 14, katika Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Mufindi Mtawalia.

Anasema, katika halmashauri tatu wanatekeleza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 50 za mwanzo kwa kila halmashauri za; Ruangwa, Mbogwe na Handeni ambazo zina mgao wa kilomita 100 kila moja.

Kanyenye anasema, mwaka uliopo wa fedha wanatarajia kuanza ujenzi katika Bonde la Mto Msimbazi, Dar es Salaam, pakitengewa Dola za Marekani milioni 270.

Anasema mradi utahusisha ujenzi wa daraja eneo la Jangwani, mfereji na barabara yake, kwamba usanifu umeshafanyika na tathmini ya mazingira imeshafanyika.


"Vilevile tunatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa kuendeleza miji 45 (TACTIC). Awamu ya kwanza tunatarajia kuanza na miji 12 ya mwanzo ya Arusha, Dodoma, Tabora, Kigoma Ujiji, Mwanza, Ilemela, Geita, Kahama, Morogoro, Mbeya, Sumbawanga na Songea. Utekelezaji wake umeshaanza," anasema.



Sehemu ya barabara iliyojenga mkoani Mbeya zote ni kazi za wakala huo. **PICHA ZOTE: TARURA.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# LATRA mnaupiga wote, lakini pigeni na hapa






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

NAONA Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) inajaribu kuupiga mwingi. Au mnaonaje wenzangu (kwa sauti ya Uhuru K.)?

Ukifuatilia kinachofanyika, utaona inahamisha watu kutoka analogi kwenda dijitali, sasa tunatakiwa tukate tiketi kwa njia ya mtandao tukitaka kusafiri kwa mabasi.

Haitoshi, naiona LATRA tofauti na iliyokuwa ile SUMA+TRA, hii inataka sasa watu wakisafiri wasafiri kwa raha bila usumbufu, kutoka kituo kimoja kwenda kingine.

Nimewasikia wakikemea tabia ya watu kupanda kwenye mabasi na kuanza kuhubiri neno la Mungu. Pia, wale wapandao na makasha yaliyosheheni vyakula na vinywaji wakinuka vikwapa na kuhanikiza kwa abiria kununua, bei yao sasa!

Nimeyafurahia haya matatu na ndiyo sababu nadiriki kusema inajaribu kuupiga mwingi, lakini kinachotakiwa ni elimu na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa yote haya.

Najiuliza, hivi wajameni (kwa sauti ya Uhuru K.), hii dijitali itawahusu na wale ndugu zetu, wazee wetu walioko vijijini na hata wasio na simu au kompyuta? Elimu imeshaanza pia huko? Tukiambizana kuwa mwisho wa mwezi huu ndio mwisho wa tiketi analojia, tutakuwa tumetenda haki mpaka kwa hao wenzetu wa nilikokusema huko vijijini? Kama utafiti na upembuzi yakinifu umeshafanyika na kuona inafaa basi na ifae, ianze.

Na tutakapoanza, tukumbuke pia kuna wenzetu wanaopandia njiani ambao naamini hawatakuwa kwenye digitali, lakini wapo wenye dharura ya safari mara moja, kuwa limezuka la kuzuka wanataka usafiri na wako njiani huko, wanafanyaje wawe kidijitali?

Hilo kwa kweli linahitaji elimu haina mwisho, ili kila mmoja aweze kujua na jinsi ya kufanya mpaka mambo yawe bulbul. Ni utaratibu mzuri tena wa kisasa, usio na usumbufu, lakini shaka yangu ni katika utekelezaji.

Lakini, kwa kuwa mwelekeo umeshaonekana hakuna linaloshindikana chini ya jua. Ili mradi kodi ya serikali inapatikana.

Tuache hilo, nirudi kwenye hawa jamaa wahubiri ndani ya mabasi mpaka kwenye d aladala, wanaodhani katika mabasi abiria wote ni waumini wao! Hili la kuwazuia ni mwafaka na swadakta kabisa.

Waacheni watu waende kwenye majumba yao ya ibada, badala ya kulazimishana kwenye mabasi ambamo kila mmoja ana lake analowaza, hajui siku itaishaje mara anaingia mtum anasikia ooh...

Mwingine anaingia na kutisha abiria, oh bila kusikia neno la ... safari hii haitakuwa na amani, hivyo sote tufumbe macho tuiombee safari yetu, kana kwamba watu walimsubiri yeye ndipo wamwombe Muumba wao, Kwani hawakuomba majumbani mwao? Wengine wakimaliza wanaomba sadaka!

We unavamia basi... unawavuruga tu na utumbo street wako walahi! Hapo Latra mmeupiga wote kabisa. Pia, wenye mabasi nao waache ile ya kutuwekea kanda za video za kiimani safari nzima, huku si wa imani tukilazimika kusikiliza.

Lingine ambalo sasa Latra mnapaswa kuliangalia, ni hili la sisi abiria wa mikoani kulazimishwa kwenda kula kwenye hoteli za wenye mabasi au maswahiba zao kwa bei ya kuua mtu.

Abiria huna hili wala lile, mara ghafla basi linachepuka barabara na kuegesha kwenye hoteli na mnatangaziwa abiria dakika 10 za kula na kuchimba dawa, mnakwenda kula bei ni kama mko sijui nchi gani, tofauti kabisa na tulikozoea kwa mama/baba n'tilie. Mnalazimika kula kwa sababu hukuna jinsi wala pengine pa kupata huduma hiyo, ila kwa ruhusa ya dereva na msaidizi wake, ambao wao kula yao ni 'kitonga', hawalipi chochote zaidi ya kupeleka wateja sisi pangu pakavu, kumchangia mwenye hoteli au basi.

Latra mkiweza kulishughulikia na hili, bila shaka mtakuwa mmeupiga wa funga mwaka, bila kutoa nje na hakika safari zitakuwa za mustarehe, kuliko hivi sasa ambapo tuna bambikiwa vitu vingi mpaka kufika unakokwenda, umekombwa sehemu kubwa ya akiba yako.

Ila hakuna lisilowezeka na kama nilivyosema hapo juu, twende kwa hatua kwa mwendo huu wa jongoo na vumbi nyuma, ipo siku yote haya yatasahaulika na kupanda basi kuwe kama kupanda ndege, kwani hakutakuwa na usumbufu wa wauza uturi, wauza korosho, mahindi ya kuchoma na mayai ya kuchemsha, na hawa longolongo wa injili.

Alamsiki!

BIASHARA

# Maonyesho ya ufugaji yalivyonoga na safari kuelekea zama za kufuga kisasa

## • Wafugaji Pwani waonyesha njia iliko



Mwenyekiti wa TCCS, Naweed Mulla, akitoa maelezo kwenye maonyesho, mkoani Pwani. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

TANZANIA inaelezwa kuwa nchi ya pili Afrika kwa ufugaji ng'ombe wakifikia milioni 35.3 mifugo mingine mbuzi milioni 25.6, kondoo milioni 8.8 na kuku milioni 92.8.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa pamoja na kuwa na idadi hiyo kubwa ya mifugo bado sekta hiyo haijachangia kikamilifu kwenye uchumi wa nchi hususani upande wa uzalishaji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema uzalishaji maziwa upo chini hasa kwa ng'ombe wa asili wanaozalisha wastani wa lita moja na nusu kwa siku na nyama wastani wa kilo 150 kwa ng'ombe mmoja.

Ndaki anasema, kutokana na kutambua hali hiyo katika sekta ya mifugo serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa kukuza sekta hiyo, ili iweze kuchangia malighafi viwanda nchini.

Aidha, serikali inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kusaidia wafugaji kupata huduma bora za ugani, ili kuwezesha kundi hilo kufuga kwa tija na kuinua kipato chao na taifa.

"Nawapongeza chama cha wafugaji ng'ombe kibiashara Tanzania (TCCS) kwa jitihada zao za kubuni maonyesho na kutoa huduma za ugani kwa njia ya maonyesho. Namna hii inawezesha wafugaji kujionea matokeo chanya na kujionea mbinu za ufugaji bora na kuchochea ari ya kufuga kwa kufuata ushauri wa wataalamu," anasema Waziri Ndaki.

Hivi karibuni chama hicho cha wafugaji ng'ombe kibiashara, kimefanya maonyesho ambayo yamewakutanisha wafugaji katika maeneo mbalimbali na kutoa fursa ya kujifunza ufugaji bora wa kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa wataalamu wa ugani.

Mwenyekiti wa TCCS, Naweed Mulla, akizungumza katika maonyesho hayo, anasema lengo hasa lilikuwa kuwaonyesha wafugaji faida za kufuga kibiashara, kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu.

Anaeleza kuwa kuna wafugaji waliokuwa na uhitaji wa kufuga kisasa, lakini hawakuwa na namna ya kujua mahali wangepata elimu ya ufugaji kwa tija,

Anasema, suala la kufanikisha maonyesho hayo ilikuwa ni ndoto ya chama anachokiongoza, kuhakikisha wafugaji wanakutanishwa na kujionea mifugo, iliyofugwa kisasa na faida zinazopatikana.

Kiongozi huyo anaiomba serikali kuendelea kushirikiana na sekta binafsi kuleta mabadiliko ya ufugaji na kuwafanya wafuge kwa tija.

"Lazima tubadilishe mbegu za ng'ombe bora na elimu yetu itajikita huko ili viwanda vya ndani viache kuchakata ng'ombe 100 kwa ajili ya nyama ya kiasi ambacho kinawezekana wakachinja ng'ombe ishirini pekee wa kisasa," anasema.

Mulla anafafanua jambo la uhamasishaji kwa sasa ni kuanza kutoa elimu na semina mbalimbali kwa wafugaji, wawe na mbegu bora ili maboresho yaendane na jitihada za serikali.

"Tunapotaka kwenda kwa pamoja watu wanatakiwa kuelewa tunaendaje kwenye ufugaji huu wa kisasa ni lazima tupeane elimu, ng'ombe bora aina ya borani katika maonyesho haya ametokea ranchi ya mbogo ambayo mimi ni mmoja wa wamiliki na ameuzwa kwa Shilingi. milioni 13," anasema

Kadhalika, anasema kupitia maonyesho hayo ya kwanza kufanyika hapa nchini yupo ng'ombe alikuwa anauzwa kwa sh.milion 40 kutokana na ubora wake na mnunuzi alikwama kwenye bei ya sh. Milion 25.

Anasema ng'ombe na mbuzi waliouzwa katika mnada huo wametoa taswira halisi ya faida za kufuga kibiashara kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu na mfugaji kunufaika na mifugo yake mwenyewe.

**AWARAI VIONGOZI**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakari Kunenge, ni kati ya watu waliotembelea maonyesho hayo, anapongeza TCCS kwa kuandaa maonyesho ambayo yataleta mabadiliko kwa wafugaji.

Kunenge anasema, ni lazima wafugaji wapate elimu na kufuga kibiashara kitendo ambacho kitakuwa na tija kwenye ufugaji wao.

Kadhalika, Kunenge anasema kufuga kisasa pia kutaondoa migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, na kwamba wafugaji wanatakiwa kutumikiwa na mifugo na si mifugo iwatumikishe na ili kuwa na mabadiliko katika soko ni lazima kujua aina ya ng'ombe wanaofaa kufugwa katika mkoa wa Pwani.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji mkoa wa Pwani, Ngobere Rashid, anaeleza kuwa maonyesho hayo yamekuwa na faida kwa wafugaji kujua namna ya ufugaji bora.

Ngobere anasema, wafugaji wengi bado wanafuga kwa njia za asili ambazo faida wanazokumbana nazo ni ndogo ukilinganisha na gharama wanazotumia.

Anasema wataendelea kushirikiana na TCCS katika kueneza elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji ili wawe na mabadiliko na kufuga kibiashara na kunufaika na mifugo yao

**ANENAYO MFUGAJI**

Jackson Mollel, ni mkazi wa mkoa wa Iringa, ambaye pia ni mmoja wa wafugaji walioshiriki katika maonyesho hayo alinunua ng'ombe kwa Sh. Milioni 9.7

Mollel anasema kilichomsukuma kununua ng'ombe huyo kwa bei kubwa ni kutokana na ubora kwake na namna ya upatikanaji wa aina kama hiyo.

"Kilichonisukuma kununua ng'ombe wale ni kutokana na ubora wake, mara nyingi kupata kama hawa ni lazima uagize nje ya nchi kumpata kwangu hapa nimeona ni bahati kubwa na itaenda kuboresha ufugaji kwenye shamba langu," anasema.

Anawasisitiza wafugaji kuwa na mabadiliko kwenye ufugaji, wajikite kutumia wataalamu na mbegu bora ili wawe na ufugaji wa tija wenye manufaa badala ya hali ilivyo sasa kwa walio wengi kutumia njia za asili.

INATOKA UK.11

# Ni uwanja mpya wa batiki wazalishaji kuunganishwa

Anasema, inataka kuwaona wanamke wakiwa na furaha siku zote na kwamba ipo tayari kuwasaidia pia vijana katika shughuli zao mbalimbali za kiuchumi.

"Rais Samia ana lengo la kuwakomboa wanawake na kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo kuwakopesha fedha kutoka katika haina za halmashauri," anasema Waziri Dorothy.

Aidha, pamoja na Rais kuwashika mkono wanawake na vijana, pia wizara yake itaendelea na utaratibu wa kuwawezesha wanawake katika kuzalisha bidhaa ili kuinua vipato vyao.

"Asilimia 75 wanaozalisha batiki ni wanawake na vijana, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuwekeza katika makundi haya, na tutaweka siku maalumu ya uvaaji batiki ambayo itakuwa ni kila Julai 8 ili kila Mtanzania avae vazi hili," anasema.

**FURSA WANAWAKE**

Waziri anasema, Rais Samia amefungua fursa kwa wanawake na kuwaonyesha kuwa wanaweza, na kwamba ni muhimu kuchapa kazi kwa kushirikiana na wanaume kuinua uchumi wa nchi. "Mfano, kutungwa kwa Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2018 inayozitaka halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo isiyo na riba wanawake wamenufaika,"anasema.

Anafafanua kuwa, mwaka 2020/21 zilitengwa Shilingi bilioni 62.68 na kufikia Juni 30, 2021, Shilingi bilioni 53.81 zilikopeshwa kwa makundi 7,993 ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ikiwa ni sawa na asilimia 86.

Dk. Dorothy anasema, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 28.17 zilitolewa kwa vikundi vya wanawake 4,894 vilivyozalisha ajira 52,428.Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe, anawataka waandaaji wa Siku ya Batiki kufanyika nchi nzima, ili kuwapa Watanzania nafasi ya kujionea.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Latifa Mohamed Khamis, analiomba Shirika la Viwango TBS, kutoa vyeti vya ubora wa bidhaa za batiki.



# Mfumo uthibiti wa ubora maji waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeanzisha rasmi matumizi ya mfumo wa uthibiti ubora wa takwimu za rasilimali za maji (QMS) ili kuboresha utendaji kazi wa bodi za maji za mabonde nchini.

Mabonde hayo ni Rufiji, Wami-Ruvu, Kati, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Mto Pangani, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Wizara ya Maji, Simon Nkanyemka, alisema hayo jana alipokuwa akihitimisha mafunzo ya matumizi ya mfumo huo yalioandaliwa na wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) pamoja na Shirika la Kimataifa la Ujerumani (GiZ) yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema mfumo huo umeanza kutumika rasmi Julai Mosi, mwaka huu na kila Bodi ya Maji ya Bonde inaendelea kutoa taarifa ya utekelezaji wake wa kila wiki.

Alibainisha kuwa lengo kuu la mafunzo ya QMS ni kuboresha utendaji wa shughuli ya msingi za mabonde ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa kutumia takwimu sahihi za wingi na ubora zitakazofanikisha kutimiza malengo ya serikali ya muda mfupi, kati na mrefu.

"Jukumu la msingi la Wizara ya Maji ni kusimamia sera na sheria katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji ya uhakika mijini na vijijini, jukumu ambalo litafanikiwa kuweka mikakati madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za maji kwa kuwa na takwimu sahihi zitakazosaidia kutimiza malengo ya wizara," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kuimarisha eneo la ukusanyaji wa takwimu sahihi za hali ya maji, hatua itakayosaidia mabonde yote kupata vyeti vya ithibati vya ubora utakaotokana ufanisi wake.

Nkanyemka alisema mfumo huo utakuwa mwarobaini wa baadhi ya kero ikiwamo ukusanyaji hafifu wa madhuhuli kupitia ukusanyaji wa takwimu sahihi za watumia maji.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Rasilimali za Maji wa wizara hiyo, Robert Sunday, alisema mafunzo hayo yamekuwa na mafanikio makubwa ambapo zaidi ya washiriki 200 wameshiriki na kufuzu mafunzo hayo.

# Serikali yaja na kampeni kabambe wanaume kushiriki malezi watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, inakusudia kuanzisha kampeni maalum ya kutoa elimu na kuhamasisha wanaume kushiriki katika malezi na makuzi ili kupunguza vitendo vya ukatili kwa watoto.

Waziri wa wizara hiyo, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo juzi alipokuwa akifungua maadhimisho ya Jubilee ya miaka 25, ya Jumuiya ya Montessori Tanzania (MCT).

Dk. Gwajima alisema takwimu zinaonyesha kuwa kuanzia Januari hadi Desemba, mwaka jana, watoto waliofanyiwa vitendo vya ukatili ni 11,499.

"Katika idadi hiyo takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 12 tuu ya watoto hao ambao kesi zao ziliripotiwa kwa vyombo mbalimbali vya sheria," alisema.

Pia alisema kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa wazazi wote wawili kushirikiana katika malezi na makuzi ya watoto ili kuwajengea misingi bora.

"Ni asilimia ndogo sana ambayo inaonyesha kuwa wanaume wanashiriki katika malezi na makuzi ya watoto hasa kwenye kushiriki mambo kama haya yanayotoa fursa kwao kuhusu malezi ya watoto, hivyo tunatarajia kuanzisha kampeni maalum ya kutoa elimu kwa kundi hili la wanaume," alisema.

Dk. Gwajima pia alisema hatua ya wanaume kushiriki katika malezi ya watoto, kitasaidia kumjengea mtoto kujiamini na kuwa na ujasiri katika kupinga ukatili.

Kadhalika, alisema malezi na makuzi ni jambo ambalo linahitaji uelewa wa hali ya juu kwa wazazi ili kusaidia kujenga misingi bora kwa watoto katika kipindi cha miaka miwili hadi minane.

"Elimu ya malezi ni jambo muhimu sana kwani katika umri huu mdogo hatupaswi kukosea kabisa. Kuna haja ya mbinu hizi wanazozitumia wenzetu wa Montessori na sisi kama serikali kuzitumia katika shule zetu kwani takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya watoto wanaharibikiwa wakiwa majumbani kwa kufanyiwa ukatili na ndugu wa karibu na asilimia 40 ni shuleni," alisisitiza Dk. Gwajima.

Mwenyekiti wa Montessori, Martha Dello, alisema suala la malezi na makuzi kwa watoto ni jambo la muhimu kwa kuwa ndilo linalomjengea misingi ambayo ataitumia akiwa mkubwa.

"Tunaposikia leo baba kambaka mtoto wa miaka minne ni msingi ambayo huyo baba alijengewa akiwa mtoto. Pia tunaposikia mama kamchoma mto mikono mtoto aliyeiba hela, tunapaswa tujiulize ni misingi gani ya malezi aliyapitia," alisema.

Jumuiya ya Montessori Tanzania (MCT), inatokana na jina la Dk. Maria Montessori mwanafalsafa ambaye alihusika kubuni zana mbalimbali za kujifunzia watoto kulingana na mazingira yao wakati wa Vita Kuu vya Dunia ya Kwanza na vya Pili.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wentworth Resources Plc, Katherine Roe (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa ripoti ya Maendeleo Endelevu ya kampuni hiyo, iliyoelekeza mipango mkakati ya mazingira, kijamii na utawala. Wengine ni Mkurugenzi Mkazi Wentworth Gas Ltd, Richard Tainton, Mjumbe wa Bodi ya kampuni hiyo, Juliet Kairuki na Rais wa Wentworth Tanzania, Bob McBean. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikoa vinara matumizi mbolea yatajwa

**Magdalena Jackson na Peter Mkwavila,** DODOMA

MIKOA sita imetajwa kuwa kinara kwa matumizi ya mbolea mashambani ikiwamo Ruvuma, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe na Rukwa huku maeneo mengi yakionekana kutumia kwa kiwango kidogo.

Kutokana na hali hiyo, wakulima wa mikoa inayotumia mbolea ya kukuzia mazao kwa kiwango cha chini imetakiwa kuongeza matumizi ili kilimo chao kiwe na tija.

Ofisa Udhibiti Ubora wa Mbolea kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Steven Gossi, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya wakulima (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Alisema kwa kushirikiana na serikali za mitaa, watahakikisha wakulima wanapata elimu sahihi ya matumizi ya mbolea na wafanyabiashara wanauza mbolea yenye ubora ili waitumie kwenye uzalishaji wa mazao.

Aidha, alisema kwa sasa serikali imetenga Sh. bilioni 150 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, hivyo wakulima nchini wachangamkie fursa hiyo kwa kusajiliwa kwenye mfumo kupitia mamlaka za serikali za mitaa na kupewa namba ya utambulisho.

Ofisa huyo alisema usajili wa wakulima kwa ajili ya kupata mbolea za ruzuku utaanza hivi karibuni ni vyema wakahakikisha wanakwenda kujisajili kwenye ofisi za serikali za kata na vijiji.

"Hii mikoa ambayo ina matumizi madogo ya mbolea wanapaswa kutambua umuhimu wake na kwa msimu huu wa mwaka 2022/23, serikali imetoa fedha hizo ili kupunguza makali ya bei ya mbolea na kuongeza upatikanaji wake," alisema.

Katika kuhakikisha kuwa ruzuku ya mbolea zinawafikia wakulima, serikali imeandaa mfumo utakaotumia programu maalum ya kidigitali kwa ajili ya kuratibu shughuli zote.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kufanya ukaguzi kwenye maduka ya pembejeo kuangalia kama yana leseni na vigezo vinavyotakiwa.

Naye Ofisa Udhibiti Ubora wa Mbolea, Salvatory Kalokola, aliwataka wakulima kujitokeza kujisajili ili wanufaike na ruzuku hiyo.





# Mbunge atoa neno kwa madiwani sensa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKATI maandalizi ya sensa yakiendelea maeneo mbalimbali nchini, Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, ameishauri serikali kuwatumia zaidi madiwani na watendaji wa vijiji na kata kwa kuwa wako karibu zaidi na wananchi.

Mwakagenda alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe juu ya ushiriki wa wabunge katika kufanikisha sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanya Agosti 23, mwaka huu.

Alisema madiwani na watendaji wanapaswa kushirikishwa kikamilifu kwa kuwa wako karibu zaidi na wananchi na wanawajua zaidi, hivyo wanaweza kusaidia sensa kufanikiwa kwa asilimia kubwa.

Pia aliwaomba waratibu wa sensa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu toafuti kati ya sensa na anwani za makazi kwa sababu maeneo mbalimbali aliyotembelea wanahoji suala hilo kujirudia mara mbili.

"Sensa ya watu na makazi ni suala muhimu sana kwa maendeleo ya taifa kwa sababu inatoa dira na mwelekeo katika kipindi cha miaka 10. Ni muhimu tukalichukulia kwa uzito unaostahili.

"Yako mambo ya kuendelea kuyaboresha ikiwamo ushirikishwaji wa watendaji na madiwani kikamilifu ili kufahamu idadi kamili ya watu sambamba na kuendelea kutoa elimu ya tofauti kati ya anwani za makazi na sensa kwani watu wanachanganya," alisema.

Aidha, Mwakagenda aliwaomba watu maarufu na baadhi ya viongozi kuacha kutumia sensa kisiasa kwa kuwa kufanya hivyo kunaweza kukwamisha jambo hilo.

Kuhusu maonyesho ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, aliwashauri kinamama kujifunza mbinu mbalimbali za uzalishaji wa mazao kutoka kwa wataalamu wa kilimo.

Alisema mbinu hizo zikiwamo za teknolojia zitawasaidia kuzalisha kwa tija na kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao wanayozalisha.




Meneja wa Benki ya Exim Tawi la Mbeya, Peter Mwamala (wa pili kulia), akizungumza na wadau wa kilimo waliotembelea banda la benki hiyo katika maonyesho ya Kilimo Nanenane yanayofanyika kitaifa katika Uwanja wa John Mwakangale, jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela miaka 30 kumbaka mtoto wa kumzaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela Ayub Jackson (34), mkazi wa kijiji cha Mlima Njiwa baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mtoto wake mwenye umri wa miaka 14.

Akitoa hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi Mfawidhi James Mhanusi alisema kosa hilo la kuzini ni kinyume cha Sheria Namba 158(1) sura ya 20 ya Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Mazoya Luchagula, alidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Aprili 2, mwaka huu, majira ya saa 3:00 wakati mama yake akiwa ametoka nyumbani.

Luchagula alidai kuwa baada ya mtuhumiwa kutekeleza tukio hilo, polisi walipata taarifa na kuanza upelelezi hatimaye kufanikiwa kumkamata Aprili 4 akiwa katika kituo cha mabasi Mbugani akijiandaa kwenda Mbeya Mjini.

Katika kujenga ushahidi wa kesi hiyo, upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi wanne, akiwamo mtoto aliyefanyiwa ukatili huo ambaye alimtambua mahakamani kama baba yake mzazi, mama, askari na daktari aliyewasilisha fomu ya namba tatu (PF3) ya polisi iliyoambatana na vipimo vilivyoonyesha mtoto kubakwa na kusababishiwa michubuko sehemu za siri sambamba na kutokwa damu nyingi.

Akitoa ushahidi wake, mtoto huyo (jina linahifadhiwa) aliiambia mahakama kuwa baba yake aitwaye Jackson, siku ya tukio, alimvuta chumbani kwake kisha kumvua nguo za ndani na kumwingilia kimwili, hivyo kumsababishia maumivu na kutokwa damu nyingi sehemu za siri.

Baada ya mama yake kurejea, alidai kuwa alimweleza kitendo alichofanyiwa na baba yake, hivyo walikwenda kutoa taarifa kwenye ofisi ya kijiji na kupelekwa kituo cha Polisi Chunya hatimaye kufanyiwa uchunguzi ambao ulibaini kubakwa.

Hakimu Mhanusi baada ya kusikiliza upande wa mashtaka, mshtakiwa ambaye awali alikana kufanya kitendo hicho, alijitetea kuwa siku ya tukio hakuwapo nyumbani bali alisafiri kwenda Mbeya na kuwasilisha tiketi za basi na kupokewa kama kielelezo. Baada ya kuzisikiliza pande mbili, Hakimu Mhanusi alisema mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, hivyo mshtakiwa ana kesi ya kujibu na hatimaye kumpatia nafasi ya kujitetea.

Katika utetezi wake, Jackson alidai kuwa ana watoto watano na wazazi wanaomtegemea, hivyo aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu huku akidai kitendo hicho kilitokana na wivu wa kimapenzi.

Mwendesha mashtaka alisimama na kudai kuwa mshtakiwa hana makosa mengine ya uhalifu lakini kutokana na kitendo alichokifanya cha kumbaka mtoto wake wa kumzaa, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia kama hiyo, huku akibainisha kuwa vitendo kama hivyo vimekithiri wilayani Chunya kwa sasa.

Hakimu Mhanusi alisema mshtakiwa alijaribu kuidanganya mahakama kwa kutoa tiketi zenye namba mfuatano jambo ambalo haliwezekani kwa basi moja kutoa namba zinazofuatana.

Kutokana na ushahidi uliotolewa na kuthibitishwa pasi na kuacha chembe ya shaka, Hakimu alisema mahakama inamtia hatiani kwa kosa la jinai namba 235 (1), 312 sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 na 158 (1) (a) sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo, kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.=

Hata hivyo, Hakimu Mhanusi alitoa nafasi kwa mshtakiwa huyo kukata rufani endapo hajaridhika na uamuzi wa mahakama hiyo.

# JKT yatoa darasa la kilimo Nanenane

**Na Renatha Msungu ,**MBEYA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limewataka wananchi kujitokeza katika maonyesho ya kitaifa ya Nanenane yanayoendelea jijini Mbeya ili kuwapata elimu katika shamba darasa la jeshi hilo lenye mazao mbalimbali.

Akizungumza baada ya kutembelea shamba hilo Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji la JKT (SUMA JKT), Kanali Petro Ngata, alisema jamii inapaswa kupata elimu ya namna ya kulima na kutunza mazao ili kupata mavuno yenye tija.

Kanali Ngata alisema jeshi hilo liko mstari wa mbele kuhakikisha linatoa elimu ya kilimo bora chenye mfano kwa jamii ndiyo maana wameweka shamba darasa ili wananchi wajifunze.

"Naomba wananchi wajitokeze katika darasa la JKT lenye mazao mchanganyiko ambalo wanaweza kujifunza ili wakalime katika maeneo yao," alisema Kanali Ngata.

Akizungumzia ongezeko la bajeti kwenye kilimo, alisema itasaidia kupanua wigo kwenye sekta hiyo ili wakulima wazidi kupiga hatua na kufanya kilimo chenye tija.

Kutokana na hilo, alisema wakulima wanapaswa kuwa mstari wa mbele kupata elimu ya namna ya upandaji mazao ya mboga na mengine ili wafanye kilimo chenye tija.

Naye Mkurugenzi wa Kilimo na Uvuvi wa JKT, Kanali Peter Rushika, alisema JKT iko mstari wa mbele kuhakikisha kilimo kinakuwa na maslahi kwa jeshi hilo na taifa kwa ujumla.

"Haturudi nyuma kwenye kilimo. Kila iitwapo leo, tunazidi kusonga mbele kutokana na teknolojia tunayotumia kwenye kilimo," alisema Kanali Rushika.

Alisema wameshiriki katika maonyesho hayo ili kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji kutokana na kuwa wemebobea katika sekta hiyo.

Kanali Rushika alisema katika maonyesho hayo, wamekuja na teknolojia mpya ya ufugaji wa samaki katika mabwawa, vizimba na matangi pamoja na kuwaongezea huduma ya upatikanaji wa samaki aina ya sato kwa urahisi katika maeneo mbalimbali tofauti na kusubiri sato kutoka Kanda ya Ziwa pekee.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nanenane, Kanali Shija Lupi, alitoa wito kwa wakulima kufika katika shamba darasa la JKT ili kujifunza namna ya utunzaji wa mazao tokea kupanda hadi kuvuna.



# TAMWA yataka katiba za vyama vya siasa kuleta usawa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimemwomba Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuangalia utaratibu utakaovitaka vyama vya siasa kubadili vipengele vya katiba za vyama vyao ili kuleta usawa katika nafasi za uongozi.

Meneja miradi wa chama hicho Zanzibar, Ali Mohamed, alisema licha ya jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanywa na wanaharakati bado wanawake wengi wameshindwa kufikia malengo ya kupata nafasi za uongozi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa majadiliano uliofanyika ofisi za chama hicho, Tunguu Zanzibar, ambao uliwashirikisha wadau kutoka asasi mbalimbali wenye lengo la kujadili changamoto za kikatiba za vyama vya siasa ambazo zinawafanya wanawake kushindwa kutimiza malengo yao.

Alisema ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ni jambo ambalo linazungumzwa kwa muda mrefu bila ya mabadiliko yanayoridhisha na anadhani kuwa kitu pekee ni msajili kuvilazimisha vyama vyote kubadili vipengele kwenye katiba zao.

"Naamini iwapo katiba zote za vyama vya siasa zitaweka wazi ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za uongozi litakuwa suala la lazima na ni wazi kuwa kilio cha wanawake cha muda mrefu kitamalizika na hatimaye wanawake wengi zaidi watashika nafasi za uongozi," alisema.


Wakichangia katika mkutano huo baadhi ya washiriki walisema zipo changamoto nyingi mbali na udhaifu wa katiba za vyama vya siasa ambazo wanawake wanakutana nazo.

Mohamed Jabir, miongoni mwa washiriki hao, alisema kutokana na mazingira yaliyoko sasa inawalazimu wanawake wanaotaka kushika nafasi za uongozi kujiongeza zaidi kielimu na kutokuwa na hofu.

Alisema kumekuwa na hofu kubwa inayowakabili wanawake wengi wasomi, wakihofia mazingira ya kazi zao au kusubiri kwa muda mrefu huku wakikosa ajira iwapo wataamua kuingia kwenye siasa za vyama vya upinzani.

"Nina wasiwasi mkubwa huenda wasomi wengi wataendelea kushindwa kuingia kwenye siasa kutokana na mazingira kutokuwa rafiki, wengi wao wana hofu kubwa," alisema.

Naye Hawra Shamte kutoka Jumuiya ya Wanawake Wenye ulemavu Zanzibar, alisema ili wanawake wengi washike nafasi kuna haja ya kila mmoja kuona suala la siasa sio la wanaume pekee badala yake ni haki ya msingi ya kila mtu mwenye akili timamu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Balozi ambaye ni Naibu Mwakilishi wa Kudumu Ubalozi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa (UN), nchini Marekani, Dk. Suleiman Haji Suleiman, alipofika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi asema kiwango cha ufaulu kinazidi kuimarika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa dhamira ya serikali yake ni kuona kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Zanzibar unazidi kuimarika kila mwaka katika mitihani yao ya taifa.

Rais Mwinyi aliyasema hayo juzi katika hafla ya chakula alichowaandalia wanafunzi waliofaulu kwa kupata daraja la kwanza katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne mwaka 2021 na Kidato cha Sita mwaka 2022, hafla iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu ya Zanzibar.

Rais Mwinyi alisema serikali itaendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwenye ujenzi wa miundombinu ya taasisi za elimu, kuzipatia vitendea kazi vikiwamo vifaa vya kusomea na kusomeshea na kutoa mafunzo kwa walimu ili wapate mbinu bora za kufundishia.

Dk. Mwinyi aliwaahidi kuwapatia kompyuta mpakato 'laptop' wanafunzi wote wa kidato cha sita na kidato cha nne waliopata daraja la kwanza wa Unguja na Pemba.

Aliwaahidi wanafunzi waliofaulu kidato cha sita wote watapata mikopo ya elimu ya juu na kusisitiza serikali itahakikisha inaiwekea mazingira mazuri bodi hiyo huku akiwaeleza kwamba wana fursa ya kutumia bodi zote mbili za mikopo ikiwamo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia ametoa nafasi za udhamini wa masomo "scholarship" kwa wanafunzi 30 waliofanya vizuri zaidi katika mitihani yao ili kuendelea na masomo katika vyuo mbalimbali.

Alitoa pongezi kwa skuli binafsi ambazo nazo zimekuwa zikifanya vizuri na kuisaidia serikali katika kupunguza mzigo wa wanafunzi katika shule zilizoko za serikali.

Naye Waziri wa Elimu, Leila Mohamed Mussa, alisema mikakati iliyowekwa na wizara hiyo katika kuimarisha sekta ya elimu huku akiwanasihi wanafunzi waliopata daraja la kwanza wa kidato cha nne na sita kujitambua na kuthamini jambo hilo walilofanyiwa na Rais.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma, akitoa takwimu za ufaulu wa wanafunzi, alisema mtihani wa kidato cha nne ulifanyika mwezi Novemba 2021 na matokeo yake yalitoka Januari 2022 ambao jumla ya wanafunzi 15,569 walifanya mtihani na 4,403 wamefanikiwa kuendelea na masomo ya kidato cha tano Julai 2022. Alifahamisha kuwa ufaulu wao ni kati ya daraja la kwanza hadi la tatu na ni sawa na asilimia 28.3, kati ya wanafunzi hao, 445 walipata daraja la kwanza sawa na asilimia 2.8, ambao 308 ni miongoni mwao ambao wamefika Ikulu.

Alisema mtihani wa kidato cha sita ulifanyika Mei 2022 na matokeo yake yalitoka mwezi Julai 2022, jumla ya wanafunzi 3,683 walifanya mitihani na 3,644 waliofaulu kuendelea na masomo kwa ngazi ya elimu ya juu katika vyuo vya ndani na nje kwa fani zote ambazo serikali itawekea kipaumbele kulingana na mahitaji yake.

Alisema kuwa kati ya wanafunzi hao, 693 walipata daraja la kwanza, 542 waliofika katika hafla hiyo ya chakula na kupata zawadi.

Alisema takwimu za ufaulu kwa kidato cha nne zimekuwa za kutia moyo mwaka hadi mwaka kwa vile kuna ishara zilizowazi za kuimarika na kuifanya Zanzibar kuwa ni mshindani halisi kwenye matokeo ya mitihani katika mikoa ya hapa nchini.

Alisema kuwa wizara inafanya jitihada kuona kuwa matokeo ya mitihani ya kidato cha nne na sita yanakuwa mazuri na yenye kupendeza na kwamba kuanzia mwaka huu, wizara hiyo inakusudia kuongeza ufaulu angalau kwa wastani wa asilimia tano kila mwaka.

"Matokeo yote haya ni mazuri sana na mara ya kwanza kutokea tangu Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, matokeo haya yamekuja chini ya uongozi wako mahiri wa Serikali ya Awamu ya Nane, ni dhahiri kuwa mafanikio yanakisi ile slogan yako ya uchaguzi kuwa 'Yajayo yanafurahisha, yajayo ni neema tupu," alisema.

## Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania watakiwa kutumia fursa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nchi za nje kuhakikisha wanazitambua na kuziainisha vyema fursa muhimu zilizoko ili zitumike kuisaidia nchi kiuchumi na kimaendeleo.

Othman aliyasema hayo jana ofisini kwake Migombani, alipokuwa akizungumza na Naibu Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, Balozi Suleiman Haji Sulemain, aliyefika ofisini kwake kumuaga akielekea kituo chake cha kazi Mjini New York, nchini Marekani.

Alisema, hivi sasa Tanzania kama zilivyo nchi zote duniani zinazingatia kutekeleza diplomasia ya kiuchumi kwa kukaribisha wawekezaji na ushirikiano wa kampuni kubwa mbalimbali katika jitihada za kukuza maendeleo hasa katika ulimwengu wa kidijitali.

Alisema Tanzania inaendelea kufunguka kiuchumi kwa kukaribisha ujuzi na mitaji katika ushirikiano wa uwekezaji ili kuifanya nchi kusonga mbele kwa kutumia faida na tija ya ushirikiano huo kutoka mataifa na jumuiya mbalimbali ulimwenguni.

Aliwataka kufahamu siasa za dunia nazo zimebadilika hivi sasa katika kuangalia mikakati ya kiuchumi kwa kugombea mitaji ya kiuchumi iliyoko na ni muhimu kwa nchi ya Tanzania kujipanga vizuri zaidi kufaidika vyema kiuchumi kupitia wawakilishi hao.

Aidha, aliwataka mabalozi pia kujitahidi kuhakikisha ushiriki wa Tanzania unakuwapo katika masuala muhimu kwa kuwasilisha taarifa za masuala muhimu nchi na kampuni mbalimbali na kutumika katika kuchangia kukuza uchumi.

Naye Naibu Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, Balozi Suleiman Haji, alisema kwamba atajitahidi kufuata maelekezo aliyopewa ili kusaidiana kwa kushirikiana na wadau ikiwamo taasisi za kikanda katika kuunganisha na kutumia fursa tofauti zilizoko duniani kuifaidisha Tanzania kwa namna tofauti.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**SEBASTIAN F. MTALEMWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye namba **C1311/0118** kilichotolewa na TANGANYIKA CAMPAS mwaka 2014. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/64408/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMMY LABAN JACKSON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3914/0033** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ALFAGEMS SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MWA/NY/RB/281113/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TUMAINI PARTSON MWANDWANI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0374/0043** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LUPATA SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MBE/MBA/RB/216850/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NEW BOOGALOO LIMITED** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T215DMS** ,CHASISS NO **ncp605005105.** Engine No **2nz4483699** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI **ARU/ARU/RB/308863/2022**

**PAVESEAL LIMITED**
**COMPANY NUMBER 97126**
**P O BOX 4**

**SPECIAL RESOLUTION DULY PASSED AT THE EXTRA ORDINARY GENERAL METETING OF MEMBERS OF PAVESEAL LIMITED HELD AT THE REGISERED OFFICE OF THE COMPANY ON THE 29th DAY OF JULY,2022 AT 09.00 A.M PRESENT.**

1. **ALEFIYAH YUSUF BHAIJEE........CHAIRPERSON**
2. **DAWOOD SEIFUDDIN BHAIJEE....SECRETARY**

The following special resolutions were duly passed

1. Members of the company **RESOLVED** that,the company be wounded up voluntary effective from29th day of july,2022
2. That,**MR.HAMZAALI AMIRALI PATWA of H.A.PATWA &CO.**be appointed as the liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing assets of the company.

We,the undersigned shareholders of the company,hereby certify the foregoing to be a true bona fide resolution passed by the company on 29th day of july,2022

ALEFIYAH YUSUF BHAIJEE
Chairperson

DAWOOD SEIFUDDIN BHAIJEE
Secretary

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**ADDAR KALEBI KESSY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YAKE YA KIWANJA **PLOT NO 312.BLOCK B.** ENGAREOLMOTONY. KWA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU TAARIFA YA POLISI **ARU/ARU/RB/309172/2022.**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

HABARI KIMATAIFA

# China, Taiwan hatarini kuingia kwenye mgogoro

**BEIJING,** CHINA

ZIARA ya Nancy Pelosi, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Marekani katika Kisiwa cha Taiwan, imelaaniwa na China hali iliyosababisha kuamuru mazoezi ya kijeshi ya baharini na majaribio ya kawaida ya makombora katika bahari ya mashariki mwa Taiwan.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, Rais wa Taiwan Tsai Ing-wen alieleza kwamba kisiwa hicho hakitarudi nyuma kutokana na tishio kutoka China, ambayo inafanya mazoezi ya kijeshi karibu na pwani ya Taiwan kulipiza kisasi kwa ziara ya Nancy Pelosi.

Wizara ya Ulinzi ya China iliahidi kuwa jeshi litachukuwa hatua kali, na mfululizo wa mazoezi ya kijeshi yatakayokizingira kisiwa hicho kuanzia jana ikiwa ni pamoja na kurusha makombora ya masafa marefu katika mlango wa Taiwan, unaotenganisha kisiwa hicho katika China Bara.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Hua Chunying, alisema kuwa mazoezi hayo yanachukua hatua muhimu na halali ili kujibu chokochoko kali za baadhi ya wanasiasa wa Marekani na watu wanaotaka kujitenga wa Taiwan.

**VITISHO VIKALI**

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na jeshi la China, sehemu ya operesheni za kijeshi zitafanyika kilomita 20 kutoka pwani ya Taiwan.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Taiwan, Sun Li-fang, alisema "Baadhi ya maeneo ya uendeshaji ya China yanaingilia maji ya eneo la Taiwan," alisema.

Aidha, Baraza la Masuala ya Bara, chombo kinachoweka wazi sera ya Serikali ya Taiwan dhidi ya Beijing, limeshutumu utawala wa China kwa kufanya kile walichokiita uonevu mbaya ambao utaathiri kwa kiasi kikubwa amani na ustawi wa bara la Asia Mashariki.

Wakati huo huo Japan ilionyesha kutiwa wasiwasi na mazoezi ya China, ikisema kuwa baadhi ya mazoezi hayo yataingilia ukanda wake mahsusi wa kiuchumi au Exclusive Economic Zone, (EEZ).

**MARUFUKU UAGIZAJI BIDHAA TAIWAN**

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na VOA kuanzia jana China ilipiga marufuku uagizaji wa matunda na samaki kutoka Taiwan na kusitisha upelekaji wa mchanga wa ujenzi kisiwani humo, kutokana na ziara iliyozua utata ya Spika wa Bunge la Marekani Nancy Pelosi.

Ziara hiyo ya Nancy aliyoifanya mwanzaoni mwa wiki hii ilibua mvutano mkubwa wa kidiplomasia kati ya China na Marekani kwa kuwa China inadai kumiliki kisiwa hicho kinachojitawala, pia inaelezwa kuwa Nancy alitua Taiwan licha ya onyo la awali kutoka China la kutotembelea eneo hilo.

Kumekuwa na ongezeko la mivutano kati ya China na Taiwan tangu Rais Tsai Ing-WEN kuchukua madaraka mwaka 2016 akidai kwamba kisiwa hicho ni taifa linalojitawala na wala siyo sehemu ya China.

Pia inabainishwa kuwa wakazi milioni 23 wa Taiwan kwa muda mrefu wameishi kwa hofu ya kushambuliwa na China lakini hofu hiyo imeongezeka zaidi wakati wa utawala wa rais Xi Jingping wa China.

**MAREKANI HAITAITELEKEZA TAIWAN**

Spika huyo wa baraza la wawakilishi la Marekani Nancy aliahidi kwamba yeye na wabunge wengine katika ujumbe wake wameonesha kuwa hawataacha kujitolea kukisaidia kisiwa hicho kinachojitawala.

**RFI/VOA**



Mbunge wa Kimilili, Didmus Barasa akimsaidia mjane kuandaa chai. **PICHA: MTANDAO.**

# Wanasiasa waibua mbinu mpya uchaguzi Kenya

**NAIROBI,** KENYA

IKIWA ni siku tatu zimebakia kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa nchini Kenya, baadhi ya wanasiasa wameacha maisha ya starehe wakiwa katika kampeni na kugeukia kusafisha vyoo, kukata mboga na kupika chai ikiwa ni juhudi za kuwashawishi wapiga kura.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na BBC mmoja wa wanasiasa aliyewafurahisha zaidi Wakenya ni Polycarp Igathe, ambaye alivaa ovaroli, buti na glavu mpya na kuchukua ndoo ya maji na kuanza kusafisha vyoo katika mji mkuu wa Nairobi.

Igathe alikuwa Naibu Gavana chini ya Mike Sonko, lakini alijiuzulu chini ya mwaka mmoja baada ya kuchukua wadhifa huo akisema ameshindwa kupata ridhaa ya gavana ya kufanya nae kazi.

Inaelezwa kuwa mwanasiasa huyo alitumia chini ya sekunde 20 kupiga deki choo kimoja huku wasafishaji wakiangalia kwa mshangao.

"Kwa muda mrefu imeonekana kama kazi chafu lakini hii ni kazi ya kuwajibika," alisema Igathe.

Taarifa ilisema wasafishaji wa vyoo katika jiji la Nairobi wanatumia deki ya kuku kuu (mopa) na ndoo kusafisha maeneo hayo ambayo wakati mwingi hutoa harufu mbaya.

Pia Igathe ambaye anagombea kiti cha ugavana wa Nairobi aliwashangaza wengi na kupigwa picha baada ya kuonekana akiosha magari na wakati akigawa vinywaji kama mhudumu katika vilabu vya burudani nyakati za usiku.

Aidha, inadaiwa kuwa mbinu yake hiyo imekejeliwa na baadhi ya watu wakisema anatakiwa kwenda kutunza watoto na kuwafanyia kazi za nyumbani badala ya hicho anachokifanya.

Kwa upande wa wachambuzi wa masuala ya kisiasa walisema kuwa hatua hizo ni mbinu ya kujenga uhusiano mwema kwa umma na wapiga kura wanazijua sana na haziwezekani kuwashawishi kupiga kura.

Igathe ni mpinzani mkuu wa Seneta wa Nairobi, Johnson Sakaja, ambaye amekuwa akitumia mbinu kama hizo kuwashawishi wapiga kura, ikiwemo kushirikisha picha mitandaoni inayomuonyesha akinunua samaki kando ya barabara, nyanya na vitunguu sokoni badala ya kwenye maduka makubwa ya kuuza bidhaa kwa jumla.

Sakaja amekuwa Seneta wa Nairobi tangu 2017 na imetajwa kuwa hilo ni jaribio lake la kwanza kuwania ugavana.

**MAONI YA WANANCHI**

Mwananchi ambaye ni mkazi wa Nairobi Anne Wambui, alieleza kwamba wanasiasa hawajui masoko yanapatikana wapi hadi kampeni zianze.

"Tunatatizika kuishi katika jiji hili lakini mtu anayenunua bidhaa katika maeneo ya bei ghali anakuja kujifanya anatuelewa anapotaka kura yetu," alisema Anne.

Ilibainishwa kuwa Mbunge wa Kimilili Didmus Barasa amekuwa akijaribu kuwavutia wapiga kura kwa kupanda bodaboda na kuacha gari lake la kifahari.

Pia alipanda toroli ambalo liliwekwa juu ya gari lake likiwa ni alama ya chama chake na limekuwa likitumiwa kuwavutia Wakenya hasa vijana wachapakazi.

Barasa pia alipigwa picha akinywa chai pamoja na wenyeji katika kibanda cha kuuza chakula kilichokandikwa kwa udongo.

Picha zingine zilimuonyesha akitumia jiko la kienyeji la kuni kumpikia chai mjane wa miaka 67 huku akionekana akiwa amevaa nguo nzuri na viatu vya bei.

Pamoja na jitihada hizo lakini inasemekana kuwa baadhi ya wananchi walionekana kutoa maoni hasi dhidi yake katika mitandao ya kijamii.

Aliyekuwa Seneta Boni Khalwale ambaye anagombea tena ugavana wa jimbo la Kakamega lililopo magharibi mwa Kenya, alitaka kuthibitisha stakabadhi zake za barabarani kwa kuchagua kung'arisha viatu vyake kando ya barabara, akila mahindi ya kuchoma huku akisubiria asafishiwe.

**BBC**

# RUVU SHOOTING, KIPANGA MAWINDONI ZANZIBAR LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kipanga inatarajia kuikaribisha Ruvu Shooting kutoka Mlandizi, Pwani katika mechi ya michuano maalumu ya kujiandaa na msimu mpya itakayofanyika leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapo.

Mchezo huo umepangwa kufanyika kuanzia saa 10:00 jioni katika mashindano hayo yaliyopewa jina la 'Pre Season Tournament' ambayo yanaanza leo kwa kushirikisha timu nne, zote za hapa nchini.

**Timu nyingine zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo ni pamoja na mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM na Chipukizi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema michuano hiyo itachezwa kwa mtindo wa mtoano na imeamuliwa hivyo kutokana na muda mdogo uliobakia kabla ya msimu mpya haujaanza.

Vuai alisema wanaamini timu zitakazoshiriki michuano hiyo zitapata nafasi ya kujiimarisha kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi Kuu Zanzibar.

"Kwa hatua ya awali ambapo ndio kwanza tunaanza mashindano haya yatachezwa kwa mtindo wa mtoano na hii ni kutokana na kuchelewa kuanza kwa michuano yenyewe lakini pia tayari wenzetu Tanzania Bara wameshatoa ratiba ya ligi, hivyo ndio maana tunataka kukimbizana na muda," alisema Vuai.

Aliongeza lengo kuu la kuandaa michuano hiyo ni kuzifanya timu shiriki kuwa imara na tayari kukabiliana na ushindani watakaokutana nao kwenye msimu mpya wa 2022/2023.

"Tunaamini malengo yetu ya kubuni kufanyika mashindano haya yatatimia, kila timu itatumia mechi hizi kujiboresha, mechi zitawapa makocha fursa ya kurekebisha idara zenye mapungufu kuelekea msimu mpya wa ligi unaokuja hivi karibuni," kiongozi huyo alisema.

Aliongeza si timu zote zina uwezo wa kuweka kambi ndani au nje ya nchi, hivyo Kamati ya Mashindano kwa kushirikiana na ZFF iliona iandae mashindano hayo yatakayosaidia kuimarisha wachezaji wa zamani na wapya waliosajiliwa.

"Tumeanza kwa kushirikisha timu nne, lakini msimu ujao tunatarajia kuwa na vilabu vingi ikiwamo vya ndani ya Zanzibar na kutoka nje," aliongeza Vuai.

Mashindano hayo yanatarajiwa kumalizika Agosti 11, mwaka huu na mechezo yote itachezwa kwenye Uwanja wa Amaan.




Wasanii wa maigizo wakiongozwa na Abdallah Mkumbila maarufu Muhogo Mchungu (kulia), wakifanya maigizo wakati wa uzinduzi wa tangazo rasmi la Sensa 2022 uliofanyika Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Taifa Queens yaendelea kuimarika*

**Khadija Mngwai na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Netiboli (Taifa Queens), Zuwena Farouk, amesema wachezaji wake wanaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Afrika na wanafurahishwa na namna walivyoimarika.

Taifa Queens inayojifua kwenye viwanja vya Chuo Kikuu jijini Dar es Salaam inatarajia kushiriki mashindano ya mchezo huo ya Afrika yatakayofanyika kuanzia Agosti 20 hadi 28, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanaamini wataenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

"Wachezaji wanaendelea vizuri na mazoezi, ninashukuru wanaonyesha nidhamu nzuri tangu tuanze kambi yetu, kila mmoja anajituma, wanaonyesha molari ya hali ya juu na jambo jema hatuna majeruhi katika kikosi chetu.

Tunashukuru kambi ni nzuri na tunapata huduma zote muhimu, mwaka huu CHANETA wamejitahidi katika hili, tunajiandaa ili twende kufanya vizuri katika mashindano haya ambayo yatakuwa na ushindani mkubwa," alisema Zuwena.

Aliongeza bado kikosi hicho hakijapata mechi za kirafiki kwa ajili ya kukiweka imara zaidi jambo ambalo bado linafanyiwa kazi na viongozi wao wa CHANETA.

Timu zitakazofanya vizuri katika mashindano hayo zitakata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia za mchezo huo ambazo zitakafanyika mwakani nchini humo.

## Pawasa ajipanga kuiondoa Malawi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni, Boniface Pawasa amesema tayari wameshaufanyia kazi ubora na mapungufu ya wapinzani wao Malawi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kupata matokeo chanya katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Afrika (BSAFCON) na kusonga mbele.

Tanzania wanahitaji kulipa kisasi katika mchezo huo wa marudiano utakaochezwa Jumapili kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam, baada ya kufungwa mabao 3-2 ugenini.

Pawasa alisema watafanya kila linalowezekana kuhakikisha hawarudii makosa yaliyojitokeza katika mechi ya kwanza ili wapate ushindi na kuwaondoa Malawi.

"Zimebaki siku chache, tumefanyia kazi kikosi chetu kwa kuangalia zaidi ubora wa safu ya ushambuliaji ya wapinzani wetu na mapungufu yao, tunahitaji kuwa makini ili kupata ushindi katika mchezo wetu huo," alisema Pawasa.

Naye Mkurugezi wa Soka la Ufukweni wa FIFA, Mtanzania Talib Hilal ambaye yuko nchini kusaidia kuinoa Tanzania, alisema timu yao iko vizuri na ana imani wachezaji watapambana kutafuta matokeo mazuri wanayoyahitaji.

## Simba Queens yajiweka sawa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi ya kirafiki itakayochezwa katika sherehe za Simba Day zinazotarajiwa kufanyika Agosti 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo mpinzani wa Simba Queens, ambao ni mabingwa mara tatu mfululizo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania bado hajafahamika.

Nkoma alisema wachezaji wake wanaendelea vyema na mazoezi na kila mmoja anaonyesha ushindani ili kupata namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

"Timu inaendelea vizuri, tuna wiki tatu tangu tuingie kambini, ila bado hatujajua tutacheza na nani, lakini tuko tayari kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema Nkoma.

Kocha huyo alisema wamefanya usajili mzuri ambao utaleta ushindani katika kikosi chake lakini amewataka wachezaji wake wadumishe nidhamu ili kutoathiri viwango vyao.

## ZISIKUPITE

### DE JONG KUTUA CHELSEA

CHELSEA wameanza mazungumzo na Barcelona kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati Mholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri 25, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United msimu huu. (***Athletic***)

### FOFANA SAFARI IMEIVA

KLABU ya Chelsea wako tayari kumpa beki Mfaransa, Wesley Fofana pauni 200,000 kwa wiki kama wanaweza kufanya makubaliano na Leicester City, ambao wanataka pauni milioni 85 ili kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Mail***)

### SESKO ATAJWA UNITED

MANCHESTER United wamefanya mazungumzo ya mapema na RB Salzburg kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Slovenia mwenye umri wa miaka 19, Benjamin Sesko. (***Sky Sports***)

### NETO NJIA MOJA

KLABU ya Bournemouth wanakaribia kumsajili kipa wa Barcelona, Neto mwenye umri wa miaka 33 kutoka Brazil. (***Telegraph***)

### HENDERSON KUTOREJEA UNITED

GOLIKIPA wa England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 25 hataichezea Manchester United tena baada ya kujiunga na Nottingham Forest kwa mkopo, kwa mujibu wa kiungo wa zamani wa Tottenham Hotspur, Jamie O'Hara. (***Talksport***)

### BRIGHTON YAMNASA COLWILL

MLINZI wa Chelsea, Levi Colwill mwenye umri wa miaka 19 anatazamiwa kujiunga na Brighton. (***football.london***)

### UDOGIE ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wameanza mazungumzo na Udinese kuhusu beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Italia, Destiny Udogie mwenye umri wa miaka 19. (***Fabrizio Romano***)

### MODRIC AMBEBA PERISIC

WINGA wa Timu ya Taifa Croatia, Ivan Perisic mwenye umri wa miaka 33 aliwasiliana na nyota wa zamani wa Tottenham Hotpusr, Luka Modric kwa ushauri kabla ya kuamua kuondoka Inter Milan kuelekea London Kaskazini msimu huu. (***Mirror***)

### SAVAGE AGEUKA LULU

KLABU kadhaa za Championship na League One vina nia ya kumchukua kwa mkopo kiungo wa kati wa Manchester United kutoka Wales, Charlie Savage mwenye umri wa miaka 19. (***Mail***)

### ANGELINO ANUKIA BARCA

MLINZI wa kushoto wa RB Leipzig, Angelino mwenye umri wa miaka 25 analengwa na Barcelona kama wakishindwa kumsajili, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31 kutoka Chelsea. (***Sport***)

### BAYERN YAMKANA KANE

OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn, ambaye alisema straika wa Tottenham na England, Harry Kane ni "ndoto yetu ya baadaye", amesema klabu hiyo ya Ujerumani haina mpango wa kumsajili mshambuliaji kwa sasa. (***90 Min***)

### BELOTTI ATAKIWA ROMA

AS Roma imetoa ofa ya kutaka kumsajili straika wa Italia, Andrea Belotti mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka Torino kipindi hiki cha majira ya joto. (***Football Italia***)

### TAVARNIER MAMBO MAGUMU

KOCHA wa Bournemouth, Scott Parker amesema dili la kumsajili kiungo wa Middlesbrough, Marcus Tavernier mwenye umri wa miaka 23 kwa sasa limefungwa. (***Teesside Live***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KOCHA HAG AMWONYA RONALDO EPL IKIANZA

## ●●● Asema mshambuliaji huyo anatakiwa kubadilika na kujiimarisha ili...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesisitiza bado kuna nafasi katika klabu hiyo kwa ajili ya Cristiano Ronaldo, lakini amemwonya mshambuliaji huyo anatakiwa kujiimarisha yeye mwenyewe.

Ronaldo ameomba kuondoka United msimu huu wa joto na alikosa mechi nyingi za maandalizi ya msimu kwa 'sababu za kibinafsi', akicheza mechi yake ya kwanza na Ten Hag ya kirafiki dhidi ya Rayo Vallecano na akaondoka baada ya kutolewa nje kipindi cha pili.

Ten Hag baadaye alijitokeza na kufichua Ronaldo hakuwa na ruhusa ya kuondoka Old Trafford mapema, akitaja tabia yake 'haikubaliki'.

Hata hivyo, kwa hali ilivyo, Ronaldo ataanza msimu mpya kama mchezaji wa United, lakini Ten Hag amemwonya mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno kujiimarisha na asiwe na uhakika wa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara. "Nadhani anaweza (kufaa)," alisema Ten Hag.

"Yeye ni mchezaji mzuri wa mpira wa miguu, amethibitisha hilo mara nyingi, lakini kila wakati unahukumiwa juu ya kile ulichonacho sasa, kile unachowasilisha sasa, ukifanye sasa.

"Timu na Cristiano mwenyewe, lazima athibitishe."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,019,3

MECHI KALI
CRYSTAL PALACE
VERSUS
ARSENAL
1 | 4.05
X | 3.47
2 | 1.84

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CALVERT-LEWIN KUIKOSA CHELSEA

**LONDON,** England

KOCHA wa Everton, Frank Lampard amethibitisha mshambuliaji, Dominic Calvert-Lewin, atakosa kuanza msimu huu baada ya kuumia goti.

Huku Richarlison akiondoka kwenda Tottenham Hotspur mapema msimu huu wa joto, Calvert-Lewin sasa ni mmoja wa washambuliaji wawili waandamizi kwenye vitabu vya Goodison Park pamoja na Salomon Rondon.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alicheza mechi 17 pekee za Ligi Kuu England msimu uliopita kutokana na jeraha la kidole cha mguu na masuala mengine machache ya utimamu wa mwili yalisumbua msimu wake na sasa Lampard amethibitisha Calvert-Lewin hatakuwapo wakati Everton itakapoanza msimu wao dhidi ya Chelsea.

"Tunatathmini jeraha la Dom," alisema Lampard.

"Hakuna muda uliothibitishwa na tunatumaini sio muda mrefu.

"Tutamkosa kwa Chelsea. Alikuwa anaonekana katika hali nzuri ya kimwili na alikuwa akifanya mazoezi vizuri sana. Ilikuwa ni jeraha la ajabu katika mazoezi, ambalo hutokea.

"Ni aibu lakini lazima tutafute suluhu ili kujiweka imara bila Dominic kabla hajarejea."



# Koulibaly afunguka sasa ni wakati kutua Chelsea

**LONDON,** England

KALIDOU Koulibaly amekiri anahisi mwaka huu umekuwa mwafaka kwake kuhamia Chelsea.

Beki huyo wa kati wa Senegal alikuwa akihusishwa na The Blues hao kwa takribani miaka sita kabla ya kukamilisha uhamisho kutoka Napoli hadi Stamford Bridge msimu huu wa joto, na kusaidia kuziba pengo la Antonio Rudiger na Andreas Christensen.

"Ni kweli muda mrefu Ligi Kuu ilinitaka nije," alisema Koulibaly akiwaambia waandishi wa habari wakati wa kutambulishwa.

"Ninaamini katika Mungu na mambo haya ndiyo wakati ulikuwa sas
Labda kabla hakuna mtu aliyekuw
tayari na Napoli hawakutaka nije.

"Mimi sio mchezaji amba
napenda kupingana na klabu yang
kuondoka. Ninaheshimu sana mn
liki na mashabiki, lakini nadha
wakati huu ulikuwa wakati mzuri w
kuondoka Napoli.

"Nilikaa miaka nane huko, waka
mwingi mzuri na wafuasi, wachez
wenzangu, klabu.

"Haikutokea lakini siku zote ni
kuwa nikihusishwa na Chelsea n
wakati huu nyota walikuwa kwen
mstari mzuri kwa hivyo niliku
hapa na nina furaha sana kujiun
na Chelsea na Ligi Kuu ya England

HABARI MICHEZO

301,493/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/22 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.29 | 3.29 | 3.09 |
| 02. 06/08/22 | 17:00 | Bristol City vs Sunderland | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 03. 06/08/22 | 17:00 | QPR vs Middlesbrough | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 04. 06/08/22 | 17:00 | Reading vs Cardiff | 2.44 | 3.18 | 2.94 |
| 05. 06/08/22 | 17:00 | Swansea vs Blackburn | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 06. 06/08/22 | 17:00 | Burton vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.33 | 2.88 |
| 07. 06/08/22 | 17:00 | Charlton vs Derby | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 08. 06/08/22 | 17:00 | Exeter vs Port Vale | 2.53 | 3.17 | 2.82 |
| 09. 06/08/22 | 17:00 | Fleetwood Town vs Plymouth | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 10. 06/08/22 | 17:00 | MK Dons vs Sheffield Wed | 2.61 | 3.21 | 2.71 |
| 11. 06/08/22 | 17:00 | Shrewsbury vs Accrington | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 12. 06/08/22 | 17:00 | Barrow vs Bradford City | 2.59 | 3.13 | 2.78 |
| 13. 06/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 14. 06/08/22 | 17:00 | Hartlepool vs AFC Wimbledon | 2.89 | 3.24 | 2.44 |
| 15. 06/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 16. 06/08/22 | 18:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 17. 06/08/22 | 21:30 | Hansa vs Arminia Bielefeld | 2.64 | 3.34 | 2.59 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 05 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 5905 | Shanghai Shenhua vs Changchun Yatai | 3.53 | 3.34 | 1.93 |
| 13:15 | 1627 | Melbourne Knights vs Green Gully | 3.29 | 3.49 | 1.96 |
| 13:15 | 5948 | Gold Coast United vs Gold Coast Knights | 2.81 | 3.74 | 2.10 |
| 13:30 | 2958 | FC Seoul vs Jeju Utd | 2.36 | 3.28 | 2.69 |
| 14:45 | 2764 | Hougang United vs Albirex Niigata (SIN) | 5.80 | 5.20 | 1.39 |
| 15:00 | 2208 | Shenzhen vs Hangzhou NG | 3.43 | 3.19 | 2.02 |
| 15:15 | 3871 | SAI Gon FC vs Hoang Anh Gia Lai | 3.65 | 3.15 | 2.05 |
| 16:00 | 3724 | Fulham U23 vs West Ham U23 | 1.74 | 4.40 | 3.60 |
| 16:30 | 2820 | Arema vs PSS Sleman | 1.52 | 3.68 | 5.88 |
| 18:45 | 5756 | Cagliari vs Perugia | 1.88 | 3.38 | 4.03 |
| 19:00 | 2757 | Udinese vs Feralpisalo | 1.32 | 4.94 | 8.67 |
| 19:00 | 3339 | Tammeka Tartu vs Flora Tallinn | 12.75 | 6.67 | 1.15 |
| 19:00 | 4131 | Randers vs Horsens | 1.88 | 3.41 | 4.01 |
| 19:10 | 2385 | Austria Vienna II vs Kapfenberg | 2.15 | 3.53 | 2.85 |
| 19:10 | 3950 | Amstetten vs Admira Wacker | 2.17 | 3.63 | 2.75 |
| 19:10 | 3962 | First Vienna vs SKN St Polten | 2.42 | 3.33 | 2.59 |
| 19:30 | 1529 | Sandhausen vs Fortuna Dusseldorf | 2.95 | 3.35 | 2.26 |
| 19:30 | 2240 | Misr Lel Makasa vs National Bank | 4.90 | 3.30 | 1.76 |
| 19:30 | 3174 | Greuther Furth vs Karlsruher SC | 1.73 | 3.86 | 4.11 |
| 20:00 | 5246 | Duisburg vs RW Essen | 2.46 | 3.39 | 2.64 |
| 21:00 | 2098 | FC Oss vs Jong Utrecht | 2.00 | 3.63 | 3.23 |
| 21:00 | 2301 | Lyngby vs Midtjylland | 4.23 | 3.83 | 1.73 |
| 21:00 | 2492 | Willem II Tilburg vs Jong PSV | 1.59 | 4.18 | 4.58 |
| 21:00 | 2914 | Vsnk Varazdin vs Dinamo Zagreb | 7.06 | 4.80 | 1.33 |
| 21:00 | 3110 | Vasas SC vs Paksi FC | 2.40 | 3.28 | 2.64 |
| 21:00 | 3238 | Den Bosch vs FC Eindhoven | 3.09 | 3.59 | 2.07 |
| 21:00 | 5112 | VVV Venlo vs Almere City | 2.84 | 3.49 | 2.24 |
| 21:00 | 5792 | NAC Breda vs Helmond Sport | 1.41 | 4.57 | 6.36 |
| 21:15 | 3078 | Neuchatel Xamax vs Yverdon-Sport FC | 2.51 | 3.39 | 2.46 |
| 21:15 | 5804 | FC Thun vs FC Aarau | 2.25 | 3.68 | 2.60 |
| 21:30 | 1396 | AS Trencin vs Zemplin Michalovce | 1.85 | 3.58 | 3.58 |
| 21:30 | 2500 | Legia Warszawa vs GKS Piast Gliwice | 1.93 | 3.29 | 3.58 |
| 21:30 | 3668 | Eintracht Frankfurt vs Bayern Munchen | 5.61 | 5.01 | 1.42 |
| 21:30 | 3986 | OKS Odra Opole vs Wisla Krakow | 3.34 | 3.24 | 2.03 |
| 21:30 | 4381 | SV Lafnitz vs Floridsdorfer AC | 2.59 | 3.42 | 2.37 |
| 21:45 | 1242 | Birmingham vs Huddersfield | 2.47 | 3.10 | 2.85 |
| 21:45 | 1489 | Treaty United vs Waterford Utd | 4.71 | 3.93 | 1.58 |
| 21:45 | 1649 | Dundalk FC vs Derry City | 2.33 | 3.19 | 2.80 |
| 21:45 | 1794 | Galway United vs Wexford Youths | 1.43 | 4.52 | 5.50 |
| 21:45 | 3086 | Queens Park vs Ayr United | 2.33 | 3.18 | 2.93 |
| 21:45 | 3147 | Brugge vs Zulte Waregem | 1.24 | 6.05 | 9.68 |
| 21:45 | 5384 | Cork City vs Athlone Town | 1.13 | 7.02 | 13.65 |
| 22:00 | 2265 | Finn Harps vs Drogheda Utd | 2.19 | 3.24 | 2.99 |
| 22:00 | 2558 | El Gouna vs Zamalek | 5.85 | 3.83 | 1.55 |
| 22:00 | 4711 | Lecce vs Cittadella | 1.60 | 3.87 | 5.23 |
| 22:00 | 5369 | Lyon vs AC Ajaccio | 1.35 | 4.93 | 7.65 |
| 22:00 | 5721 | Crystal Palace vs Arsenal | 4.05 | 3.47 | 1.84 |
| 22:15 | 2123 | Kordrengir vs Fjolnir | 2.31 | 3.53 | 2.60 |
| 22:15 | 4597 | Sampdoria vs Reggina | 1.45 | 4.24 | 6.66 |
| 22:15 | 5425 | Benfica vs FC Arouca | 1.18 | 6.44 | 14.10 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KAGERE ASAINI SINGIDA BIG STARS MIAKA MIWILI

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Singida Big Stars itakayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu 2022/23, imefahamika.

Kagere ni miongoni wachezaji wapya waliosajiliwa ndani ya timu hiyo akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake na Wekundu wa Msimbazi kumalizika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugezi wa Ufundi wa Singida Big Stars, Ramadhani Nsanzurwimo, alisema Kagere kwa sasa ni mchezaji halali wa timu yao baada ya pande mbili hizo kufikia makubaliano.

Nsanzurwimo alisema Mnyarwanda huyo aliwasili mkoani Singida tangu juzi usiku na kukamilisha taratibu za kujiunga na klabu hiyo iliyobadilishwa jina kutoka DTB FC.

"Kagere amefunga zoezi la usajili katika klabu yetu ambayo imejiimarisha kufanya vizuri katika msimu wa 2022/23. Ni mchezaji halali wa Singida Big Stars, usajili wake uliotokana na mapendekezo ya benchi la ufundi," alisema Nsanzurwimo.

Aliongeza ujio wa Kagere katika timu hiyo utaimarisha kikosi chao katika safu ya ushambuliaji ambayo ilikuwa inaongozwa na Amissi Tambwe ambaye ni mfungaji wao bora katika timu hiyo.

"Msimu huu tumeamua kufanya kweli hakutaki kurudia makosa ya wenzetu waliopita kwa msimu mmoja kupanda na kushuka, tumedhamiria kufanya kweli kwa kusajili wachezaji wazuri na wazoefu," Nsanzurwimo alisema.

Singida Big Stars itaanza kampeni za kuwania ubingwa wa Bara kwa kuwakaribisha Tanzania Prisons katika mchezo utakaofanyika Agosti 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida.



Wachezaji wa Timu ya Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU) wakicheza dhidi ya kikosi cha Wanafunzi wa Chuo cha Madaktari cha KCMC katika mechi ya fainali ya Ligi ya Kikapu Mkoa wa Kilimanjaro iliyochezwa kwenye viwanja vya MoCU mapema wiki hii. **PICHA: JAMES LANKA**

# Polisi TZ yafurahia kuanza na Yanga

**Na Adam Fungamwango**


KIKOSI cha Polisi Tanzania kimesema kiko tayari kuwakabili mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Yanga katika mechi ya raundi ya kwanza ya ligi hiyo itakayochezwa Agosti 16, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

**Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Frank Lukwaro, alisema wameiona ratiba hiyo na kikosi chao kimeshaiva kwa ajili ya kuanza mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo itakayoshirikisha timu 16.**

"Tunaendelea vyema na kambi yetu ya maandalizi ya msimu mpya, tupo hapa hapa Dar es Salaam, tunaendelea kujifua, ratiba tumeiona, tumeanza kujiandaa na hilo, tutacheza mechi za kirafiki ili kujiimarisha zaidi. Tunaendelea pia na usajili, vitu hivyo vyote vinafanyika kwa wakati mmoja. Itakumbukwa tumeacha wachezaji wengi pamoja na kocha, tumesafisha banda na tunaingiza vifaranga wapya," alisema Lukwaro.

Aliongeza kwa usajili ambao wameufanya wana uhakika msimu ujao kikosi cha Polisi Tanzania kitakuwa cha 'kutisha'.

"Msimu ujao pale kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi, mashabiki wetu watafurahia kandanda litakalokuwa linapigwa, tumemsajili Jamal Mtegeta kutoka Dodoma Jiji na 'mtoto Idd', huyo ni Idd Kipangwile, lakini kuna straika Mkenya, Ambore Awio ambaye alikuwa Biashara United," alitamba msemaji huyo.




Kocha Hag amwonya Ronaldo EPL ikianza UKURASA 21





Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akizungumza katika uzinduzi rasmi wa mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi (UMITASHUMTA) na Sekondari (UMISSETA) uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba SC yarejea, yaileta St. George

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Simba kikirejea nchini jana kutokea Ismailia, Misri, mabosi wa timu hiyo wamewaalika St. George kutoka Ethiopia kwa ajili ya mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa Jumatatu kwenye sherehe za Simba Day.

Baada ya kutua nchini, wachezaji wa timu hiyo waliruhusiwa kurejea katika familia zao na leo wataingia kambini kuendelea na maandalizi ya Tamasha la Simba Day.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha St. George kitawasili nchini kesho tayari kwa mchezo huo na wanaamini watawapa mazoezi sahihi wachezaji wao.

Ahmed alisema baada ya kumtambulisha kiungo Mnigeria, Nelson Okwa aliyetokea Rivers United, bado imebaki nafasi moja ya mchezaji wa kigeni na usajili wake utamalizika wakati wowote kuanzia sasa.

"Usajili bado haujakamilika. Baada ya kumtangaza Okwa, tutashusha mwamba mwingine, nadhani kabla ya Ijumaa haijamalizika saa 6:00 usiku tutakuwa tumeteremsha mchezaji mwingine, halafu baada ya hapo tutaangalia kama tuendelee au tusiendelee," alisema Ahmed.

Kuhusu Mohamed Ouattara kutoonekana kambini Misri kwa muda mrefu na kutocheza mechi yoyote ile, alisema alirejea kwao nchini Ivory Coast kwenda kukamilisha ibada ya ndoa.

Wakati huo huo viongozi na mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi wameendelea kurejesha asante kwa jamii baada ya jana kukitembelea Kituo cha Watoto Yatima cha UMRA kilichoko Magomeni jijini na kukabidhi unga, sabuni, sukari, mafuta ya kupikia na taulo za watoto.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema wanafahamu wanakwenda katika msimu mgumu hivyo wanahitaji dua ili kufikia malengo yao.

Naye Issa Maeda kutoka Aliminium Profile alisema wakiwa kwenye kilele cha miaka 13 ya kuanzishwa kwao wameamua kuungana na Simba ili kusherehekea miaka hiyo kwa kujitoa kwa ajili ya jamii.

# Nabi awatuliza Yanga

## ●●● Afunguka bado hajasaini mkataba mpya huku akiendelea kupokea ofa kutoka...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anaendelea kupokea ofa kutoka katika timu mbalimbali za nje ya Tanzania lakini kwa sasa amechagua kufanya kazi katika klabu hiyo licha ya mkataba wake kumalizika.

**Nabi alitua nchini tangu Aprili mwaka jana na msimu uli omalizika amekinoa kikosi cha Yanga kwa mafanikio, ambapo amewasaidia kutwaa ma kombe matatu ambayo ni la Ligi Kuu Tanzania Bara, Ngao ya Jamii na Kombe la FA.**

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Nabi, alisema bado yuko katika mazungumzo na mabosi wa Yanga na endapo watafikia makubaliano atasaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia hapo Jangwani.

Nabi aliitaja Kaizer Chiefs inayoshikiri Ligi Kuu Afrika Kusini ni moja ya timu zinazohitaji huduma yake lakini hajachukua uamuzi wa kuondoka.

"Nimefanya mazungumo na Yanga, bado sijasaini mkataba nao ingawa nimekubali kuendelea kuifundisha timu," alisema kwa kifupi kocha huyo raia wa Tunisia.

Kocha huyo aliongeza bado yuko nchini na hana haraka kufanya uamuzi kutokana na kuamini uwezo wake.

"Mashabiki wasiwe na wasiwasi juu yangu bado nipo Yanga kwa sababu mazungumzo yanaenda vizuri na muda wowote naweza pata mkataba kuendelea kukinoa kikosi cha Yanga, kwa sasa mashabiki watulie kuona timu yao," alisema Nabi.

Aliongeza anaridhishwa na hali ya kikosi chake huku akifurahishwa na matokeo waliyopata katika michezo ya kirafiki waliyocheza ambayo imempa mwanga na mwelekeo wa yale anayoyafundisha.

"Tulianza kwa kushinda mabao 5-0 dhidi ya Transit Camp na jana (juzi), tumeshinda 2-0 dhidi ya Namungo, ni mwanzo mzuri naamini tutakuwa vizuri," alisema Nabi.

Taarifa zilizopatikana kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema Nabi anatarajiwa kupewa mkataba ambao atakuwa analipwa mshahara wenye thamani ya Dola za Marekani 50,000 (zaidi ya Sh. milioni 110 za Tanzania) wakati Kaizer Chiefs yenyewe imemtengea kiasi cha Dola za Marekani 40,000 (zaidi ya Sh. milioni 90).

Chanzo hicho kinasema Nabi hakutakiwa kurudi Tanzania baada ya kwenda mapumziko lakini alirudi kutokana na makubaliano na uongozi wa Yanga kuendelea vizuri.

"Kila kitu tayari kimekamilika kwa kocha huyo, lakini bado hajasaini kwa sababu viongozi wanahitaji ushindi katika mchezo wa Ngao ya Jamii na sherehe za Wiki ya Wananchi imalizike, maandalizi yanawaweka bize sana," kilisema chanzo chetu.

Yanga inatarajia kuikaribisha Vipers SC kutoka Uganda katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa utakaochezwa kesho kwenye kilele cha Wiki ya Wananchi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >